# Nipashe

Jumatatu Juni 15, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580258

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## PM amwagiza Ndalichako madai unyanyasaji wa kijinsia vyuoni

UK. 8




UKURASA 11

# Msigwa ataja mambo 3 urais

- Ikiwa Chadema itampa baraka za kugombea Oktoba... *Uk. 2*





Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Idd (kulia), akimsikiliza Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, wakati wa makabidhiano ya mabati 216 na mbao 333 kwa ajili ya shule tatu za awali katika Jimbo la Kikwajuni Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar, yaliyotolewa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

## KIBANO H'SHAURI MIL. 37/- KUDURUFU NYARAKA

UKURASA 3

## Zitto, Lipumba watoa bajeti mbadala

UKURASA 2, 18

### BAA LA CORONA



Suala la unawaji mikono na maji tiririka au kutumia kitakasa mikono ili kuepuka maambukizo ya ugonjwa wa corona, linapaswa kufanyika kwa umakini. Tunapaswa kusafisha mikono vizuri na sabuni kwa kuosha kiganja chote taratibu mpaka sehemu za ndani za kucha na juu ya vidole ili kuondoa vijidudu, vivyo hivyo ukitumia kitakasa mikono 'sanitizer'. WHO

- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play
Download on the App Store



MICHEZO **EYMAEL: NAFASI YA PILI MUHIMU** UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Acharazwa viboko 12 kwa kubaka mwanafunzi

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemuhukumu mkazi wa Kata ya Nyengedi, Kassimu Bidhali Chilumba (18), kuchapwa viboko 12 makalioni, baada ya kupatikana na kosa la kumbaka mwanafunzi.

Mtuhumiwa hiyo alimbaka mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Nyengedi (jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu wa Mahakama hiyo, Magala Muyonga, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, ambapo mshtakiwa alikiri kutenda kosa.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa kama ana sababu zitakazoishawishi mahakama isimpe adhabu kali, kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza, ibirisi wa mapenzi ndiye aliyemshawishi kufanya yote hayo, hivyo anajutia, huku akiahidi kutorudia kosa.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Muyonga alimuuliza mwanasheria wa serikali kama ana kumbukumbu ya makosa ya zamani ya mshtakiwa na kujibu hana, ingawa aliiomba Mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine wenye na tabia hiyo.

Hakimu Muyonga akitoa hukumu katika Shauri hilo namba 512020, kupitia vifungu vya sheria 130 (i) (2) (e) na 131 (2) (a) Sheria ya Elimu mwaka 2019, alisema amesikiliza maombi za pande zote mbili na kumuhukumu mshtakiwa Chilumba kuchapwa viboko 12 makalioni.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, kuwa mshtakiwa alimbaka mwanafunzi huyo wa kidato cha tatu Juni 5, mwaka huu, majira ya alasiri.

Mramba alidai mtuhumiwa alikamatwa eneo ambalo kinajengwa choo kipya, kilichokuwa kinajengwa nyumbani kwa mzazi wa mtuhumiwa, wakati mwanafunzi huyo akiwa anapita eneo la nyumba hiyo.

# Mch. Msigwa ataja mambo matatu urais

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Iringa Mjini (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa, ametangaza rasmi nia ya kuwania nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, kama chama chake kitampa ridhaa.

Alitangaza nia hiyo jijini Dodoma jana, huku akibainisha vipaumbele vyake vitatu ikiwamo kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu.

Msigwa, aliyabainisha hayo alipozungumza na waandishi wa habari, na kusema taifa lolote duniani ili kufikia maendeleo, ni lazima lifanye mapinduzi makubwa ya kielimu na kiteknolojia.

Alisema akipata ridhaa ya kuchaguliwa kuwa Rais atаunda serikali itakayofumumua mfumo wa elimu nchini na kuunda upya ili kupata wasomi wenye maono, maarifa, ubunifu na ujuzi mahususi wa kutekeleza malengo ya kupata matokeo sahihi ya maendeleo.

"Pia nitahakikisha kuwa serikali yangu inaachana na elimu inayopimwa kwa vyeti pekee na kuanzisha mfumo wa elimu utakao fungamanisha moja kwa moja na shabaha za maendeleo tunazolenga kufikiwa katika kila sekta, mageuzi haya makubwa ya kielimu yatakwenda sambamba na kukuza maarifa, ujuzi, teknolojia kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika sekta zote zinazohusika na uchumi na maendeleo," alisema Msigwa.

Pia, alisema binafsi anajisikia vibaya, kuwa na Profesa wa uchumi nchini ambaye hana uchumi harafu anawafundhisha wengine wawe na uchumi, au kuwa na mhandisi aliyesoma, lakini hana uwezo wa kutengeneza hata pambu ya maji kuisaidia jamii yake.

"Lakini haya yote siyo makosa yao, bali ni mfumo wa elimu ya taifa letu, lengo langu ni kujenga nchi ya wavumbuzi wa mambo ya maendeleo, kujitegemea kiteknolojia, kujiajiri na kujitegemea kifikra wanaodadisi na kutafuta uvumbuzi wa kitaalamu dhidi ya kero na matatizo mbalimbali," alisema Msigwa.

"Katika serikali yangu mimi, mapinduzi ya elimu pamoja na teknolojia ndiyo vitakuwa vitu muhimu sana ili kubadili fikra za wananchi kwa kuwa maendeleo yanaletwa na fikra sahihi pamoja na mwelekeo sahihi," alisema Msigwa.

Pia alisema Taifa haliwezi kufanikiwa katika jambo lolote kama watu wake wataendelea kuwa na fikra ndogo, kwani maendeleo ya mtu hayawezi kuzidi kiwango chake cha fikra hata mara moja.

"Kwa hiyo jambo la kwanza kama tunafikra ndogo tutapata mafanikio madogo, kiwango cha fikra tulichonacho katika uchumi ndicho hicho kitakacho tuamulia aina ya maendeleo yetu hakuna njia ya mkato msingi wa maendeleo ni fikra tofauti zetu na mataifa mengine si rangi bali ni fikra zetu tulizonazo," alisema Msigwa.

Alisema katika karne ya 19, ndipo mapinduzi ya viwanda yalianza kujitokeza kutokana na watu kuanza kufikiri, kudadisi na ugunduzi wowote umekuja kutokana na watu kuanza kuhoji, lakini hapa nchini watu wakihoji wanaonekana kuwa sio wazalendo.

Mchungaji Msigwa alisema pia kipaumbele chake cha pili, ni utawala bora na uwajibikaji kwani kukosekana kwa vitu hivyo kumekwamisha kwa kiasi kikubwa jitihada nyingi za kusukuma maendeleo ya nchi.

"Mathalani kilimo kinachoajiri Watanzania wengi kimepuuzwa na kuporomoka si kwa sababu serikali haina fedha za kutosha, bali kwa sababu tuu serikali imepuuza na kuacha kutoa fedha za kutosha zilizoidhinishwa na bunge kwa ajili ya kilimo," alisema na kuongeza:

Akipata ridhaa anakusudia kuiongoza nchi katika mageuzi makubwa, pamoja na mambo mengine atahakikisha kuwa kuna Mahakama, Bunge na taasisi huru ya kuzuia na kupambana na rushwa isiyo ingiliwa na serikali katika shughuli wala maamuzi yake.

Alifafanua kuwa, kupitia mchakato wa Katiba mpya ataimarisha mgawanyo wa madaraka na kuhakikisha kuwa kuna mifumo imara ya kuwajibisha dhana ya utendaji wa serikali.

Kadhalika, alisema kipaumbele chake cha tatu, ni mageuzi makubwa ya kiuchumi.

Aidha, alisema analenga kufumua mfumo wa uchumi, ulipo nchini na kuleta mfumo wa uchumi wa soko jamii katika nchi, ambao unalenga kuleta maendeleao shirikishi na endelevu kwa kila mtu.



Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, Peter Msigwa (Chadema), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma (hawapo pichani), wakati akitangaza nia ya kugombea nafasi ya urais kupitia chama chake katika uchaguzi mkuu ujao. **PICHA: PETER MKWAVILA**.

# Vipaumbele 5 bajeti ya ACT

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeweka bayana vipaumbele vyake vitano itakavyovizingatia kwenye bajeti watakayoiandaa watakapoongoza nchi, mojawapo ni kurekebisha muundo wa makato kutoka kwenye mapato ya waajiri na wafanyakazi ili kuchochea matumizi kwenye uchumi.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akichambua bajeti ya serikali ya mwaka 2020/21 iliyowasilisha bungeni mwishoni mwa wiki na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

"Hii ni pamoja na kutambua rasmi kibajeti malimbikizo ya kupanda mishahara kwa wafanyakazi wa umma tangu mwaka 2016 na kuweka utaratibu wa kulipa malimbikizo hayo kwa wafanyakazi wote ikiwamo wale waliostaafu ambao mafao yao yataboreshwa kwa kuzingatia marekebisho ya mishahara yao," alisema Zitto.

Pamoja na mambo mengine, Zitto alisema jambo litakalofanywa na ACT-Wazalendo kwenye bajeti ni kufanya uchambuzi wa kina kwa kutumia wataalamu wa ndani na wa nje kuhusu namna bora ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo, kwa kuingia ubia na sekta binafsi.

"Miradi mikubwa kama reli, ndege na umeme tutaingia ubia na sekta binafsi kwa kuzingatia muda wa miradi kuanza kuzalisha mapato ya kulipia madeni ya ununuzi na ujuzi wake, lengo la uchambuzi huu ni kuiondoa serikali kwenye angalau asilimia 50 ya gharama za utekelezaji ili kuelekeza rasilimali fedha kuhami maisha ya wananchi," alisema Zitto.

Alisema ACT-Wazalendo pia watatunga sera za kikodi ili kuhami sekta ya utalii na mnyororo wake ambao umeathiriwa na ugonjwa wa corona, pamoja na kulinda ajira za wafanyakazi na kampuni za utalii kwa kutoa ruzuku kwa kampuni zote zitakazoendeleza mikataba, na waajiri na kuruhusu wafanyakazi waliokosa kazi kulipwa fao la kukosa kazi kutoka mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Kuweka vivutio vya kibajeti na kikodi kwenye miradi yote ya kilimo cha umwagiliaji na viwanda vyote vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo," alisema Zitto.

Alisema ACT-Wazalendo itaweka mazingira bora ya mradi muhimu na wa lazima wa Mchuchuma na Liganga kuanza mara moja.

Kuhusu viwango vipya vya kodi, Zitto alisema ACT-Wazalendo itahakikisha mapato ya jumla yasiyozidi Sh. 420,000 kodi yake itakuwa sifuri. Mapato ya Jumla yanayozidi Sh. 420,000, lakini hayazidi Sh. 720,000, kodi yake itakuwa Sh. 36,000 + asilimia tisa ya kiasi kinachozidi Sh. 420,000.

Alisema kwa mapato ya jumla yanayozidi Sh. 720,000, lakini hayazidi Sh. milioni1.44, kodi yake itakuwa Sh. 72,000 + asilimia 15 ya kiasi kinachozidi Sh. 720,000. Mapato ya jumla yanayozidi Sh. milioni 1.44, lakini hayazidi Sh. milioni 2.88, kodi itakuwa Sh.144,000 + asilimia 20 ya kiasi kinachozidi Sh. milioni 1.44.

Alisema kwa mapato ya jumla yanayozidi Sh. milioni 2.88, lakini hayazidi Sh.milioni 15. kodi itakuwa Sh. 288,000 + asilimia 25 ya kiasi kinachozidi Sh. milioni 2.88, na mapato ya jumla yanayozidi Sh. milioni 15,000,000 kodi itakuwa Sh. milioni tatu + asilimia 30 ya kiasi kinachozidi Sh. milioni 15.

HABARI KITAIFA

# Kibano kwa h'shauri kutumia mil. 37/- kudurufu nyaraka

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MKUU wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, ametoa siku 14 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime kujibu hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ikiwamo kutolewa maelezo juu ya namna ilivyoidhinisha matumizi ya Sh. milioni 37 kudurusu nyaraka (photocopy).

Malima alitoa agizo hilo wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani kujadili hoja za CAG, ambapo alisema alishangazwa na jinsi watendaji wa halmashauri waliidhinisha matumizi hayo makubwa katika matumizi ya kupiga chapa pekee.

Katika taarifa hiyo, CAG alibaini upungufu huo, ambapo katika majibu ya msingi ya halmashauri walilipa kiasi hicho katika mwaka 2018/19 baada ya mashine zote saba zinazotumiwa kudaiwa kuharibika na kulazimika kutafuta huduma hiyo kwa gharama hiyo kwa watoa huduma binafsi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa, maelezo hayo hayakujitosheleza, na kwamba kiasi cha fedha kisichofikia hapo kingeweza kutumika kununulia mashine zingine saba kwa gharama ya Sh. milioni 2.8 kila moja kulingana na bei ya soko hivi sasa.

Licha ya kutumika kiasi hicho kudurufu nyaraka pekee, pia halmashauri hiyo ilidaiwa katika ripoti ya CAG ya mwaka 2018/19 kutenga Sh. milioni 20 kutengeneza mashine hizo, ambapo mbili pekee zilitengemaa, hatua ambayo ilionyesha kumkasirisha mkuu wa mkoa.

"Haiwezekani kutumia kiasi hicho tena kwa watoa huduma binafsi na ukifanyika uchunguzi pia ubainishe mtoa huduma huyo ili ifahamike kwa kuwa fedha hizo ni za umma," alisema Malima.

Katika hatua nyingine Mkuu huyo wa Mkoa alisema maelezo kamili ya namna ambavyo halmashauri hiyo imekuwa ikidaiwa madeni zaidi ya Sh. bilioni moja yakiwa ni malimbikizo ya mishahara ya watumishi wakati inapokea zaidi ya Sh. bilioni moja kila mwaka kutoka mgodi wa North Mara kama ushuru wa huduma.

"Naagiza manejimenti ya halmashauri kuleta majibu ya haraka na sahihi yakionyesha mkakati wa namna ya kulipa madeni hayo ambayo ni makubwa ukilinganisha na utajiri wa halmashauri hii kuliko zote mkoani hapa," alisema Malima.

Halmashauri hiyo inayoongozwa na madiwani wengi kutoka Chadema licha ya kupatikana na hoja 41 za ukaguzi ikiwamo kufanya malipo bila viambatisho katika ripoti ya CAG ya mwaka 2018/19, ilidaiwa kutumia vibaya zaidi ya Sh. bilioni 30 zilizotolewa na mgodi wa North Mara katika ripoti ya kamati ya uchunguzi iliyoundwa na mkuu wa mkoa miaka miwili iliyopita.




Dk. Lilian Mwakyosa (kulia), kutoka Shirika la Vijana nchini (Tayoa), akisisitiza jambo kwenye mjadala wa Timiza Malengo 2020 ulioandaliwa na Tayoa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ulioendeshwa kwa mtandao wa Zoom na kishirikisha wanafunzi 680 na wakuu wa taasisi 32 za elimu ya juu mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Katikati ni Dk. Siraji Shaaban wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi (NACP) na kushoto ni mwezeshaji wa mjadala huo, Stella Adams. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Hadhari ya kasi maambukizo VVU

**Na Joseph Mwendapole**

WATANZANIA wamekumbushwa kuwa makini wasipate maambukizo ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa Ukimwi (VVU), kwani takwimu zinaonyesha kuwa kila dakika moja Watanzania wanne wanapata maambukizo mapya.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Jeremia Mushi kutoka Mpango wa Taifa wa Kupambana na Ukimwi (NACP), kwenye mjadala ulioandaliwa na Shirika la Vijana nchini Tayoa, jijini Dar es Salaam.

Mjadala huo wa 'Timiza Malengo 2020' ulifanyika kwa njia ya mtandao wa Zoom ulishirikisha wanafunzi 680 na wakuu wa vitivo 40 kutoka taasisi 32 za elimu ya juu nchini uliandaliwa na Tayoa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na NACP.

Wengine waliochangia mjadala huo wenye lengo la kuwafanya vijana kutimiza ndoto zao kwa kujilinda dhidi ya maambukizo ya VVU ni Kampuni ya Vodacom, Tigo, Zantel, Halotel, Airtel, TTCL, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Shirika la Afya na Utafiti wa Tiba la Afrika (AMREF).

Mushi alisema hadi sasa Watanzania milioni 1.7 wamethibitika kuwa na maambukizo ya VVU na asilimia 95 ya hao wanatumia dawa za kufubaza virusi hivyo, huku kila mwaka watu 72,000 wakipata maambukizo mapya.

Alisema takwimu zinaonyesha kila mwezi watu 6,000 hupata maambukizo mapya wakati kwa siku watu 200 hupata maambukizo hayo na wanne hupata maambukizo hayo kila dakika moja.

Naye Eda Charles kutoka NACP, alisema wasichana wengi wanajikuta wakipata ujauzito na wengine kushindwa kutimiza ndoto zao kutokana na mazingira magumu yanayowakabili wanapokuwa shuleni kwani wengi wao hulazimika kutembea umbali mrefu kufika shuleni.

"Wasichana wanakosa mahitaji muhimu sasa watu wazima wanaowatamani hutumia mwanya wa changamoto zinazowakabili kuwapata na mwisho wa siku wanaweza kuambukizwa VVU au kupata mimba wasizotarajia na kukatisha ndoto zao," alisema Eda.

Mratibu wa Umati, Fredi Turuka, alisema vijana wengi wamekuwa wakiogopa zaidi kupata mimba, lakini wanadharau kuvaa kinga wakati wa kujamiiana jambo ambalo limekuwa likichangia kuongezeka kwa maambukizo mapya.

# Wenye majengo, ardhi ya kupangisha wabanwa kodi

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imewataka wamiliki wa majengo, fremu na ardhi kuwaruhusu wapangaji wao kukata asilimia 10 ya kiasi cha malipo walichokubaliana katika mkataba wa upangishaji ili waiwasilishe TRA.

Ofisa Msimamizi Mkuu wa Kodi wa TRA, Stephen Kauzeni, aliyasema hayo wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi eneo la Tabata jijini Dar es Salaam.

Alisema kodi ya zuio inatozwa kwa mujibu wa sheria ya kodi ya mapato na inasimamiwa na TRA, hivyo aliwataka wapangishaji kuwaruhusu wapangaji wao kuzuia kodi hiyo wakati wanapolipwa kodi ya pango.

"Tangu tumeanza zoezi hili la elimu kwa mlipakodi, tumefanikiwa kupita karibu maeneo yote ya Tabata, katika maeneo yote haya tumegundua kwamba, baadhi ya wamiliki wa nyumba za biashara hawaruhusu wapangaji wao kukata kodi ya zuio ambayo inapaswa kuwasilishwa TRA kwa mujibu wa sheria," alisema Kauzeni na kuongeza:

"Tulichokifanya ni kuwaelimisha wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kodi hiyo, napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa wenye nyumba na fremu mbalimbali kuwaruhusu wapangaji wao kuzuia asilimia 10 ya kiasi cha malipo walichokubaliana kwenye mkataba wa upangishaji, ili wapangaji hao wakiwasilishe TRA."

Rashid Omary, ambaye anamiliki fremu za biashara eneo la Tabata Kimanga alisema amefurahishwa na elimu ya kodi ya zuio aliyoipata kutoka kwa maofisa wa TRA na aliwaomba wamiliki wenzake kuhakikisha wanawaruhusu wapangaji wao kuzuia asilimia 10 ya kodi ya pango ili fedha hizo ziwasilishwe TRA kama sheria inavyoelekeza.

"Kama mimi ni mmiliki, lakini nilikuwa sielewi kama wapangaji wangu wanatakiwa kunikata asilimia 10 ya kodi ya pango tuliyokubaliana kwenye mkataba ili waipeleke TRA. Hivyo elimu hii imenifungua sana na hivyo napenda kuwashauri wamiliki wenzangu wawaruhusu wapangaji wao kukata hiyo asilimia 10 kwa sababu kodi hii itarudi kwetu kupitia maendeleo yanayoletwa na serikali katika maeneo yetu tunayoishi," alisema Omary.

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**EDWARD NZELA MBAGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya mitsubishi yenye namba za usajili **T 808 BZD.** Chassis No. **FK61BMZ510025,** Engine No. **6D17790505.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/444287/2020.**

115773902

# 'Tiba asili marufuku ramli chonganishi'

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, amepiga marufuku waganga wa tiba asili kupiga ramli chonganishi kwa madai kwamba wanawasaidia wananchi.

Dk. Mollel alisema serikali inatambua mchango mkubwa unaofanywa na waganga hao, lakini kufanya ramli chonganishi ni kwenda kinyume na taratibu na miongozo ya serikali.

Alisema hayo jana, wakati wa hafla fupi ya wahitimu wa mafunzo ya uboreshaji wa utoaji huduma za tiba asili iliyohudhuriwa na baadhi ya wawakilishi kutoka Wizara ya Afya na wanafunzi wa taaluma ya uuguzi Mirembe jijini Dodoma.

"Mambo ya ramli chonganishi, hayatakiwi katika nchi yetu, kitu tunachosisitiza ni tiba kwa kutumia mimea yetu ambayo Mungu aliiumba, ambayo ni mimea ya chakula, ya matunda na mimea dawa. Hiyo ndio tunataka mkaiibue huko mlete itusaidie kutibu watu wetu," alisema.

Pia alikemea tabia ya baadhi ya waganga hao kutumia imani potofu katika taaluma ya tiba hiyo.

"Hatutegemei mtu atuambie jiwe litutawale, hizo imani ambazo mtu anatawaliwa na jiwe, mtu anatawaliwa na hirizi, sisi tunataka tiba ambayo sisi binadamu tutatawala vitu vyote na imani potofu isisogelee kabisa kwenye utaratibu wetu wa tiba asili," alisisitiza.

Alisema serikali inawatambua na itaendelea kushirikiana na wataalamu wa tiba asili na tiba mbadala kutokana na kuwa na mchango chanya katika kuwahudumia wananchi hasa katika kipindi hiki ambacho nchi na dunia kwa ujumla imepitia changamoto ya maambukizo ya virusi vya corona.

Mwenyekiti wa wahitimu wa uboreshaji wa tiba hizo asili, Dk. John Lupimo, alisema wao kama wataalamu wa tiba asili, wataendelea kushirikiana na serikali ili kuikuza taaluma hiyo hususan katika kipindi hiki cha ugonjwa wa corona.

# Tathmini ya TPSF bajeti 2020/2021

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi nchini (TPSF), imeipongeza bajeti ya mwaka 2020/21 ambayo ilisomwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, wiki iliyopita kwa kujielekeza zaidi katika kupunguza gharama za uzalishaji, kufanikisha utekelezaji wa 'Blue Print' na kulinda viwanda vya ndani.

Akizungumza jijini Dar es salaam mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, mbali ya kuipongeza serikali kwa kuja na bajeti hiyo, na kwamba imegusa maeneo mengi muhimu katika sekta mbalimbali za uchumi na kujikita zaidi katika kuinua maisha ya Watanzania.

"Katika bajeti hii tumeona serikali imeainisha vipaumbele vyake katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa kutoa asilimia 37 ya bajeti, kitu ambacho kitachochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa sekta ya viwanda, uzalishaji na ajira na hatimaye kujenga uchumi imara na endelevu," alisema Ngalula.

Alisema kuwa ukuaji wa uchumi wa nchi unategemea uwapo wa taasisi binafsi ambayo hutafsiri yaliyomo kwenye bajeti kwenye maisha ya kawaida, hivyo amewataka wadau wa sekta hiyo, kutumia mazingira hayo mazuri kuzidi kufanya biashara na kuwekeza zaidi.

"Unafuu wa kodi na kufutwa kwa tozo mbalimbali kunafanya mazingira ya biashara na uwekezaji kuwa katika hali nzuri, hivyo natoa wito kwa wawekezaji wazawa kutumia fursa zilizoainishwa katika bajeti hii ili kukuza mitaji yao, kuongeza mzunguko wa biashara na kutengeneza ajira kwa Watanzania."

Aidha, Ngalula alisema kuwa bajeti hiyo imeonyesha mwanga kwa taifa kupunguza hali ya utegemezi katika kushughulikia masuala ya ndani ya uchumi wa nchi hasa katika kipindi hiki ambacho dunia nzima inapambana na janga la ugonjwa wa Covid-19.

"Serikali kupitia Rais John Magufuli imekuwa ikihimiza umuhimu wa kujitegemea na hasa kipindi hiki ambacho ugonjwa wa Covid-19 umeikumba dunia. Wito wangu kwa wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani kuitafsiri dhana ya kujitegemea kwa vitendo katika maeneo ya vifaa tiba/kinga, usafirishaji wa anga wa mizigo, chakula na kuzalisha malighafi za viwandani," alieleza Ngalula.

Aidha, alisema hatua ya serikali kupendekeza kutolewa kwa tozo 60 za udhibiti kutarahisisha zaidi shughuli za ufanyaji biashara na uwekezaji.

"Kilio cha wafanyabiashara na wawekezaji ni uwapo wa tozo nyingi ambazo zilikuwa kikwazo, kuondolewa kwa tozo hizo 60 kutasaidia wadau wa maendeleo kujihusisha zaidi na uwekezaji na biashara hali ambayo itachangia ukusanyaji wa kodi na kutengeneza ajira kwa vijana wa Kitanzania," alisema na kuongeza: TPSF itaendelea kuwaunganisha wadau wake na serikali ili kufikia azma ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025."



Tangi la maji lenye uwezo wa kubeba lita 75,000 linalojengwa na Shirika lisilo la kiserikali la People`s Development Forum (PDF) kwa Sh. milioni 153.9 litakalotatua changamoto ya ukosefu wa huduma ya majisafi na salama kwenye wodi ya mama na mtoto. **PICHA: SHABAN NJIA.**

# Haki Fursa yachambua bajeti za EAC

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Haki Fursa, limeichambua bajeti ya Tanzania mwaka 2020/21, kwa kulinganisha na nchi za Afrika Mashariki, kuwa ni yenye kuwajali wananchi wake na italeta mageuzi makubwa.

Aidha, imempongeza Rais John Magufuli kwa kuongoza vyema mapambano ya corona kwa kuwa na ujasiri wa kukataa kuifunga nchi, jambo ambalo limewezesha wananchi kuendelea na shughuli zao na kupunguza athari kwenye uchumi.

Wakizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Haki Fursa, Ntimi Charles, alisema bajeti hiyo imeweka vipaumbele kwenye maeneo yanayogusa maisha ya watu.

Maeneo hayo ni kuondoa umaskini, kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana, kuendeleza vita dhidi ya rushwa kwa vijana, kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, kuendeleza kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya watu na mali zao.

Alisema bajeti hiyo imeweka mkakati wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, kugharamia shughuli za serikali ikiwamo miradi mikubwa ya kimkakati na uboreshaji wa huduma za kijamii kwa lengo la kuleta maendeleo kwa haraka.

Akilinganisha na bajeti za nchi za Afrika Mashariki, alisema Tanzania kwa bajeti ya Sh. trilioni 34.88 inaonyesha upekee katika ukuaji wa uchumi ikizingatia huduma za jamii na haina utegemezi.

"Huduma za jamii ikiwamo elimu, afya, huduma ya majisafi na salama pamoja na miundombinu ya barabara viliwafikia wananchi kwa kiwango cha kuridhisha," alisema.

"Sisi kama shirika linalojihusisha na maendeleo tuliona upatikanaji wa mahitaji ya msingi kwa wananchi kumepungua kutoka asilimia 28.2 mwaka 2011/2012 hadi asilimia 26.4 mwaka 2017/18, huku kina cha umaskini kulipungua kutoa asilimia 6.7 hadi 6.2 kipindi hicho," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, serikali imedhibiti matumizi yasiyo ya lazima, mianya ya rushwa na kujielekeza katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha, alichambua bajeti za nchi nyingine na kuonyesha kwa Kenya inakabiliwa na mdororo wa uchumi kutokana na corona, huku bajeti ya elimu, bunge na idara za mahakama ikipungua, na kwamba wameendelea kukopa nje ambako kunaongeza mzigo kwa nchi.

Kwa upande wa Uganda, ajira za vijana zitaathiriwa kutokana na kodi kubwa na kutowekeza kwenye miundombinu, huku serikali ikiendelea kukopa nje ili kufikia malengo ya kibajeti.

Kwa upande wa Rwanda, alisema wanapanga kukuza uchumi kwa kutumia mikopo, ruzuku, viza, faini za trafiki na leseni, na watalazimika kukopa zaidi kwa ajili ya kujikwamua kutokana na athari za corona.

"Tunampongeza Magufuli kwa kutokubali nchi kufungwa kwa sababu ya corona, hii imesaidia uchumi wetu haujaathirika sana," alisema Ofisa Mipango wa Haki Fursa, Reuben Kwagilwa na kuongeza:

"Bila ujasiri huo tungeingia kwenye mtego wa kufunga nchi na kuteteresha usalama wetu na maziwa makuu kwa kuwa sisi ni njia kuu ya kutoa huduma kupitia bahari na maziwa."

**TANGAZO**

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED

## AUDITED FINANCIAL STATEMENTS

**ISSUED PURSUANT TO REGULATIONS 7 AND 8 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014**

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31ST DECEMBER 2019

(Amount in thousands shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2019 | Previous year 31st Dec 2018 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 1,391 | 8,057 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 237,751 | 431,181 |
| 3 | Investments in Government securities | - | - |
| 4 | Balances with other banks and financial institutions | 1,128,056 | 1,979,765 |
| 5 | Cheques and items for clearing | - | (107,289) |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probable losses) | 223,571 | 377,305 |
| 12 | Other assets | 40,513 | 129,152 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 1,165,698 | 1,229,188 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **2,796,979** | **4,047,359** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 5,431,542 | 5,139,155 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | 339,210 | 338,053 |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | 16,441 | 40,772 |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | 58,825 | 19,060 |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 580,013 | 180,478 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| **29** | **TOTAL LIABILITIES** | **6,426,031** | **5,717,518** |
| **30** | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **(3,629,052)** | **(1,670,160)** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 6,529,002 | 7,363,802 |
| 32 | Capital reserves | 453,542 | 453,542 |
| 33 | Retained earnings | (9,585,337) | (6,873,651) |
| 34 | Profit (Loss) account | (1,048,296) | (2,623,756) |
| 35 | Other capital accounts | 22,037 | 9,903 |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| **37** | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **(3,629,052)** | **(1,670,160)** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 1,529,827 | 1,615,762 |
| 40 | Allowances for probable losses | 1,257,800 | 1,272,968 |
| 41 | Gross Loans and advances | 1,559,250 | 1,716,357 |
| 42 | Other non performing assets | 79,128 | 66,083 |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | -129.75% | -41.27% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 98.11% | 94.14% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 27.02% | 31.34% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 7.99% | 9.32% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 38.45% | 32.26% |
| (vi) | Deposits Growth | 5.69% | -47.79% |
| (vii) | Assets growth | -30.89% | -52.81% |

### STATEMENT OF COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2019

(Amount in thousands shillings)

| | | Current Year 31st Dec 2019 | Previous Year 31st Dec 2018 |
|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 58,041 | 295,320 |
| 2 | Interest Expense | 102,353 | 243,212 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **(44,312)** | **52,108** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | (15,168) | 1,198,260 |
| **6** | **Non Interest Income:** | **107,771** | **78,743** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 35,268 | 74,335 |
| | 6.3 Dividend Income | - | - |
| | 6.4 Other Operating Income | 72,503 | 4,408 |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **1,126,923** | **1,556,347** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 517,513 | 590,830 |
| | 7.2 Fees and Commission | 49,536 | 58,753 |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 559,874 | 906,764 |
| **8** | **Operating Income/ (Loss)** | **(1,048,296)** | **(2,623,756)** |
| **9** | **Income Tax Provision** | **0** | **0** |
| **10** | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **(1,048,296)** | **(2,623,756)** |
| **11** | **Other Comprehensive Income (itemize)** | | |
| **12** | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | | |
| 13 | Number of Employees | 22 | 32 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | 0 | 0 |
| 15 | Number of Branches | 1 | 1 |
| **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | 0.39% | 0.39% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | -1.65% | -1.65% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 670.49% | 78.40% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | -2.32% | 1.70% |

### STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 31ST DECEMBER 2019

(Amount in thousands shillings)

| | | Current year 31st Dec 2019 | Previous year 31st Dec 2018 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income (Loss) | (1,048,296) | (2,623,756) |
| | **Adjustments for:** | | - |
| | - Impairment/Amortization | 24,385 | 10,838 |
| | - Prior Year Adjustment | 12,134 | (40,686) |
| | - Depreciation | 63,489 | 63,489 |
| | - Net change in Loans and Advances | 153,734 | 3,061,472 |
| | - Gain/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | 293,544 | (4,704,366) |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | | |
| | - Net change in Other Liabilities | 439,300 | 47,387 |
| | - Net change in Other Assets | 64,252 | 710,240 |
| | - Tax Paid | | |
| | - Others (specify) | | |
| | - Due to other banks | (24,331) | 25,987 |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **(21,789)** | **(3,449,395)** |
| **II:** | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purcharse of Fixed Assets | - | - |
| | Proceeds from Sale of Fixed Assets | - | - |
| | Purchase of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Proceeds from Sale of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Others (Adjustment on Property Plant and Equipment) | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | **-** | **-** |
| **III:** | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Long Term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | (834,800) | 5,851,306 |
| | Payment of Cash Dividends | - | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others (specify) | (87,928) | (3,015,291) |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Activities*** | **(922,728)** | **2,836,015** |
| **IV:** | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **(944,517)** | **(613,380)** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **2,311,714** | **2,925,094** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **1,367,197** | **2,311,714** |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 31/12/2019

(Amount in thousands shillings)

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | General Provinsion Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at 1st January, 2018** | **1,512,496** | **-** | **(3,858,359)** | **93,021** | **27,594** | **453,543** | **-1,771,705** |
| Profit for the year | - | - | (2,623,757) | - | - | - | -2,623,757 |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 5,851,306 | - | - | - | - | - | 5,851,306 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | | (83,925) | - | - | (83,925) |
| General Provision Reserve | - | - | | - | (26,787) | - | (26,787) |
| Others | - | - | (3,015,292) | - | - | - | (3,015,292) |
| **Balance as at 31st December, 2018** | **7,363,802** | **-** | **(9,497,408)** | **9,096** | **807** | **453,543** | **(1,670,160)** |
| | | | | | | | |
| **Balance as at 1st January, 2019** | **7,363,802** | **-** | **(9,497,408)** | **9,096** | **807** | **453,543** | **(1,670,160)** |
| Profit for the year | (834,800) | - | (1,048,296) | - | - | - | (1,883,096) |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | - | - | (87,929) | - | - | - | (87,929) |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | | 12,644 | - | - | 12,644 |
| General Provision Reserve | - | - | | - | (511) | - | (511) |
| Others | - | - | | - | - | - | - |
| **Balance as at 31st December, 2019** | **6,529,002** | **-** | **(10,633,633)** | **21,740** | **296** | **453,543** | **(3,629,051)** |

The above extracts are from the financial statements of the Bank for the year ended 31st December,2019 which have been prepared in accordance with International Financial Reporting Standards (IFRS).The financial statements were audited by MUHASIBU CONSULTANTS and received a qualified report.The financial statements were approved by the Board of Directors on 15th June, 2020 and signed on their behalf by:

| *Name* | *Signature* | *Date* |
|---|---|---|
| 1. Dr G Machimu, **CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS** | …………………….. | **15th June 2020** |
| 2. Ms A.A. Mshana , **VICE CHAIR PERSON BOARD OF DIRECTORS** | …………………….. | **15th June 2020** |

215773602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi michuano ya Afrika yaanze mapema

**WAKATI** Ligi Kuu Tanzania Bara ikirejea tena baada ya kusimama kwa zaidi ya miezi miwili ili kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona (Covid- 19), klabu zinatakiwa kukumbuka maandalizi ya msimu mpya.

Ligi Kuu Tanzania Bara imerejea katika viwanja mbalimbali nchini, huku ikiwa tayari hatua ya lala salama imeingia.

Lala salama au wengine hupenda kuita mechi za funga pazia, hii ni ishara sahihi kwamba kinachofuata baada ya ligi hiyo, ni timu zetu kwenda katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Ligi Kuu yenyewe hutoa tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati bingwa wa michuano ya Kombe la FA, yeye hupata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Maandalizi ya msimu mpya yanatakiwa yaangalie kuimarisha vikosi kwa ajili ya mashindano ya ndani pamoja na michuano ya kimataifa.

Nipashe inazikumbusha timu zote ambazo zina nafasi ya kupata tiketi hizo, kuanza na kufikiria maandalizi ya kupeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano hayo ya kimataifa kwa upande wa Bara na Zanzibar.

Lakini hata timu ambazo haziko kwenye mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara au Kombe la FA, bado zinatakiwa kujipanga kuhakikisha zinasajili wachezaji wenye ubora ambao watawapa matokeo mazuri katika msimu ujao.

Viongozi wa timu wanatakiwa kuongeza umakini katika kuviimarisha vikosi vyao pamoja na benchi la ufundi kwa kuzingatia ushindani watakaokutana nao kwenye michuano ya kimataifa kwa kusajili wachezaji watakaoendana na hadhi ya mashindano hayo.

Klabu yenye kufikiria kutwaa mataji, ni lazima ikubali kuwekeza katika kipindi hiki kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu na wenye uzoefu wa kukabiliana na ushindani kwenye kila mchezo.

Ifike mahali, timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara au Ligi Kuu Zanzibar ziwe na uwezo wa kuwania taji hilo na kukataa kujiona wao ni wasindikizaji.

Tunawakumbusha ili Timu ya Taifa (Taifa Stars), iwe na kikosi imara, ni lazima klabu zinazoshiriki Ligi Kuu kusajili wachezaji wenye viwango bora na ambao wanaweka mipango ya kuziandaa timu hizo kushindana.

Timu zitakazojiandaa vizuri kuelekea msimu mpya, inamaana zitakapopata tiketi ya kuiwakilisha nchi katika mashindano ya kimataifa, zitakwenda kushindana na si kushiriki kama zilivyozoeleka.

Maandalizi mazuri, yatazifanya timu za Tanzania kuonyesha ushindani kwenye mashindano hayo ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa kuwa na uhakika wa kutinga hatua ya robo au kutinga hatua ya mbele zaidi.


Kama inavyoaminika kuwa matokeo mazuri ya soka hayatokani na 'miujiza', basi ni vyema klabu zetu zikafanya maandalizi sahihi na kujihakikishia nafasi ya kupeperusha vizuri bendera ya Tanzania kwenye mashindano ya kimataifa na kuacha kuitwa wasindikizaji.

Mbali na kufanya vizuri, pia jina timu ndogo au 'under dog' pia litakuwa msamiati adimu, pale vigogo wa michuano hiyo watakapokuwa wanakutana na timu za hapa nchini.

Hakuna kisichowezekana, kama leo hii tunashuhudia Taifa kama Madagascar limekuwa likifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa kwa nchi kujipanga vema, basi hata klabu za Tanzania zinaweza kubadili taswira kwa kuwekeza katika kiwango cha juu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera wasimamizi U/Kambarage, lakini...



Na Adam Fungamwango

**LIGI** Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, imesharejea ili kumalizia mechi zilizobaki, baada ya kusimama kwa muda kutokana na janga la ugonjwa wa Covid-19.

Serikali ilisimamisha rasmi michezo Machi 17, mwaka huu, ili kupambana na ugonjwa huo, lakini baada ya juhudi za kutosha zilizofanyika na kupungua kwa ugonjwa huo, michezo iliruhusiwa tena kufanyika kuanzia Juni Mosi.

Hata hivyo, serikali bado ikasisitiza kuwa pamoja na kuruhusu michezo, na kuruhusu pia mashabiki kuingia viwanjani, lakini taratibu zote za kuingia uwanjani na kukaa zifuatane na kanuni za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mwadui dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga na Coastal Union dhidi ya Namungo FC kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga ndizo zilikuwa timu za kwanza kufungua dimba baada ya mapumziko ya corona kumalizika.

Kabla mechi ya Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga, zilisambaa picha zikionyesha kitu ambacho hakijapatwa kushuhudiwa huko nyuma.

Ni kwamba kwenye majukwaa kuliwekwa alama nyeupe kuonyesha kuwa hapo ndipo anatakiwa kukaa mtu mmoja.

Alama hizo zilikuwa zikiachana mita moja kabla ya nyingine, ina maana mtazamaji mmoja akikaa katikati ya alama hiyo, atakayekaa mwingine mbele yake, nyuma, au pembeni yake, itakuwa pia ni mita moja, kwani nako pia kuna alama nyingine.

Nilichoshuhudia muda huo ni kwamba mashabiki walikuwa wameitikia wito, kila mmoja akiwa kwenye sehemu yake aliyopangiwa.

Kwa hili niwapongeze sana wasimamizi wa Uwanja wa Kambarage, na hata Chama cha Soka Mkoa wa Shinyanga, na hata wenyeji wa mchezo huo, Mwadui FC.

Kama ni kufuata masharti yote ya afya, uongozi wa Uwanja wa Kambarage umekuwa ni mfano wa kuigwa na viwanja vingine vyote inafaa vifanye hivyo.

Hata askari polisi wa Shinyanga nao wanastahili pongezi, kwani nao walionekana kuwa makini kuangalia zaidi mashabiki kuliko mpira kama inavyokuwa huko Ulaya.

Hata hivyo nina wasiwasi na uwanja ulivyojaa baadaye kama hali hiyo ilifuatwa.

Na si kama uwanja huo ulijaa sana, ila mashabiki walionekana kujirundika eneo moja la jukwaa, huku eneo lingine likionekana halina watu, lingine likiwa na watu wachache.

Hii ina maana hapa sasa si tatizo la uongozi wa uwanja bali ni mashabiki wenyewe.

Mashabiki wa soka mara nyingi wana tabia ya kupenda kukaa pamoja, kuliko kukaa mbalimbali na hii inatokana na asili yenyewe ya soka ambayo mbali na kabumbu kuchezwa uwanjani, lakini huambatana na maneno ya kejeli, vijembe, mipasho, na hata maneno ya kutiana moyo au kulaumiana wenyewe kwa wenyewe, ambayo yote hayo mashabiki wanakuwa wamekaribiana.

Kama chochote kibaya kitakachojitokeza kwenye Uwanja wa Kambarage, basi wa kuliaumiwa watakuwa ni mashabiki wenyewe na si uongozi wa uwanja ambao wamejitahidi na kufanya kila kitu ilichobidi wafuanye na vingine zaidi ambavyo wengi tuliona ni vipya kabisa.

Mimi nadhani ifike mahali mashabiki nao wahakikishe wanajilinda wenyewe, kwa kutapakaa uwanjani na si kujirundika sehemu moja kama ilivyoonekana Kambarage.

Wala si serikali, Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi, wala polisi wanaoweza kulinda afya na uhai wa mtu, bali unaanzia kwa mtu mwenyewe kwanza.

# Wataalamu UDSM watafiti chemchemi kwenye stendi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WANASAYANSI 'nguli' watano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wameanza utafiti wa kina kuchunguza kiini cha chemchemi kuibuka chini ya majengo ya mradi wa kimkakati wa kituo kikuu kipya cha mabasi yaendayo mikoani na nje ya nchi.

Kituo hicho kinajengwa katika eneo la Ngangamfumuni, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Mradi huo wa kimkakati, unajengwa na kampuni ya ujenzi ya kimataifa ya CRJE (East Africa) Ltd ya China.

Jana, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mbobezi wa utafiti wa Geo Fizikia, Dk. Simon Melchioly, alithibitisha kuwa chuo hicho kimepeleka wanasayansi wake Moshi Mjini, kwa ajili ya kufanya utafiti huo na kushauri nini kifanyike ili kunusuru stendi hiyo isiishie njiani.

"Baada ya kuona tukio hili la chemchemi zimeibuka ghafla na zinamwaga maji mengi ndani ya stendi inayojengwa hapa Moshi, Makamu Mkuu wa Chuo alituagiza kama chuo tuje tutoe mchango wetu kama watu wa Jiolojia. Tumekuja timu ya watu watano, watatu ni watu wa technical (ufundi), kwa ajili ya kufanya Geological (utafiti wa kijiolojia) na Geo-Physics na Hydrogeological Studies," alisema.

Ujenzi wa mradi huo unaotekelezwa kwa awamu tatu, uliidhinishwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi). Kituo hicho kikuu cha mabasi cha Ngangamfumuni, ujenzi wake utaigharimu serikali zaidi ya Sh. bilioni 27.

Dk. Melchioly alieleza kuwa lengo lao kama wataalamu ni kuzunguka pande zote za majengo hayo kujua miamba iliyoko chini, iko vipi na kama kuna uwezekano wa kuwa na njia za maji.

Akizungumza na wataalamu hao, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema amewaelekeza kukaa pamoja na wataalamu wengine, wawaeleze njia rahisi ambayo serikali inaweza kuitumia kuhakikisha maji yanayotokana na chemchemi hizo yatatoka.

"Njia binafsi ambayo nafikiri mimi ni kuyaelekeza haya maji kutoka na yakaungane na maji mengine kutoka maeneo mengine kwenda Mto Njoro. Maji yaliyoingia kwenye hilo jengo jipya yanaanza kuonyesha athari ya kulizuru, kama hatutawahi kuyaondoa.

"Kwa hiyo kuna aina mbili ya maji yaliyopo ndani ya mradi huo, kuna maji yaliyopo ndani yanayotokana na chemchemi zinazotoka chini, halafu kuna maji yanayoonekana yanakuja kutoka juu, na yanakula ukuta wa hili jengo kwa nyuma, kwa kiwango ambacho maji yanakwenda mpaka yanaanza kuchuruzika kwenye ukuta wa ndani. Maana yake yamefanikiwa kupenya kwenye ukuta wa nje ambao ni mpana."

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Mkoa, kwa sasa kazi kubwa ni kuzuia maji ya nje yasiingie kwenye ukuta na kuingia ndani, na yale yaliyoko ndani na yenyewe yatafutiwe njia yatoke nje.

## Katibu AMCOS ashtakiwa madai uhujumu uchumi

**Na Happy Severine**, SIMIYU

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Wilaya ya Itilima mkoani Simiyu, imemfikisha mahakamani Katibu wa AMCOS ya Mwanga kituo cha Nangale, Masanja Mabula kwa kosa la uhujumu uchumi.

Mabula alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Simiyu, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Venance Mlingi, akishtakiwa kwa kughushi Sh. milioni saba, wizi wa Sh. milioni 12 na kusaababishia mamlaka hasara ya Sh. milioni 22.5.

Kupitia kesi namba 23/2020, Mabula alisomewa mashtaka hayo na Mwendesha Mashtaka wa Serikali mkoani hapa, Amani Mohamed.

Ilidaiwa kuwa Elia mshtakiwa, alipokea Sh. milioni 221 kutoka Kampuni ya NGS Investment Co. Ltd ya Majahida, Bariadi ili akalipe wakulima waliouza pamba kwenye AMCOS ya Mwanga kituo cha Nangale na kwamba alilipa baadhi ya wakulima, lakini shilingi milioni 22.5 alitoroka nazo kwenda mkoani Singida.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Juni 24, mwaka huu itakapotajwa tena mahakamani hapo na mshtakiwa huyo amerudishwa rumande kutokana na mashtaka ya uhujumu uchumi kutokuwa na dhamana.



Uchafu ukiwa umezagaa katika Soko la Buguruni Dar es Salaam, jambo ambalo ni hatari kwa wananchi wanaoingia kupata mahitaji. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Vyama visivyo na wabunge kushirikiana uchaguzi Oktoba

**Na Gwamaka Alipipi**

UMOJA wa vyama vya siasa visivyo na wawakilishi bungeni, vimetangaza kushirikiana katika uchaguzi mkuu, kwenye ngazi ya ubunge na udiwani, kwa kufanya kampeni pamoja.

Vyama hivyo ni DP, NRA, AFP, UMD, UPDP, Demokrasia Makini, TLP, UDP, SAU, NLD, ADC, na CCK, ambavyo vimeamua kusimamisha wagombea kwenye uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mratibu wa umoja huo, Rashid Rai alisema: "Tunatangaza kushirikiana katika uchaguzi mkuu kwenye ngazi ya udiwani na ubunge, tutasimamisha mgombea kwenye kila jimbo".

Kuhusu nafasi ya mgombe urais, Rai alisema kila chama kitafanya mkutano mkuu na kuamua namna ya ushirikiano na kwamba vitatoa matamko kuhusu nafasi hiyo.

Aidha, aliitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kuhakikisha inakuwa macho katika kuwakamata na kudhibiti vitendo vya baadhi ya wagombea ambao wamejiandaa kutoa rushwa kwa wananchi.

Alisema rushwa ni mojawapo ya mambo yanayoharibu uchaguzi mkuu, na kwamba wagombea wasiokuwa na sifa ndiyo wanaochaguliwa kwa kutoa rushwa.

"Tumemsikia Katibu Mwenezi na Itikadi wa Chama Cha Mapinduzi, Humprey Polepole, akizungumzia masuala ya rushwa katika chama chake, tunamwomba suala la rushwa lisiishie katika uteuzi tu, bali waendelee hadi kwenye ngazi ya uchaguzi," alisema na kuongeza:

"Tunataka suala la kupinga rushwa liende hadi kwenye sanduku la kupiga kura, suala la kupita bila kupingwa nalo tutalihesabu kama sehemu ya rushwa kwa sababu haiwezekani mgombea apite bila ya kupingwa," alisema Rai.

Mwenyekiti wa umoja huo, Hassan Almas, alisema kwenye kila jimbo vyama vyao vitashirikiana kwa kupiga kampeni kwa pamoja na kwamba kila mgombea atakapokuwa anafanya kampeni atakuwa na bendera za vyama vyote.

Alisema kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu, umoja huo umeamua kusimamisha mgombea kwenye kila jimbo, na kwamba watahakikisha mgombea atakayeteuliwa kukiwakilisha chama amechaguliwa na wajumbe wa vyama vyao.

Naye Katibu wa umoja huo, Abdul Mluya, akizungumzia kuhusu tukio la vyama vya siasa kusaini maadili ya uchaguzi alisema: "Tulisaini pasipo kulazimishwa, sisi tulisaini baada ya kuona maadili yapo vizuri, sasa hao wanaolalamika kwamba walilazimishwa tunawashangaa."

Alisema wakati wa kusaini maadili hayo hakuna chama kilicholazimishwa, na kwamba baadhi ya vyama wanataka kufanya mchakato wa uchaguzi kuwa ni suala la kwao peke yao, jambo ambalo siyo kweli kwani ni suala linalowashirikisha wananchi.

Aidha, aliwataka Watanzania kuwa makini na wagombea watakaowafuata wakati wa kampeni na kuwaomba kura kwa sababu wengi wao watakuja na hoja za udanganyifu.

# PM amwagiza Ndalichako madai unyanyasaji vyuoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema matukio ya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanafunzi wa vyuo vikuu yamepungua, huku akimwagiza Waziri wa Elimu, Prof.Joyce Ndalichako, kusimamia kuanzishwa kwa madawati ya malalamiko vyuoni.

Aidha, ameagiza Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais, Tamisemi, kuwatambua wanafunzi wenye vipaji na vipawa vya masomo ya sayansi.

Kauli hiyo aliitoa jana katika hafla ya kuweka jiwe la msingi na kupokea Shule ya Wasichana ya Bunge iliyojengwa katika eneo la Kikombo jijini hapa.

Alisema serikali itaendelea kuchukua hatua kali kwa wahadhiri wanaowafanyia unyanyasaji wa kijinsia watoto wa kike vyuoni kwa kuwalaghai ili kuwapatia ufaulu mzuri.

Alimpongeza Prof. Ndalichako kwa kuendelea kuchukua hatua na sasa matukio hayo yanapungua.

"Wizara ya Elimu hakikisheni madawati ya jinsia yanafunguliwa katika vyuo vikuu nchini ili kuwasaidia wanafunzi wa kike kuweza kuripoti pindi wanapopata matatizo ya kiunyanyasaji," alisema.

Alisema idadi ya wanafunzi wa kike kwenye vyuo vikuu imeongezeka ambapo kwa mwaka 2010/11 walikuwa 49,959 na hadi mwaka 2017/18, walikuwa 90,159.

Aliagiza kudhibiti utoro na mimba kwa wanafunzi huku akisisitiza serikali itachukua hatua kwa wale wote watakayokatisha ndoto za watoto wa kike.

"Nyie vijana mtoto wa kike aachwe aende kusoma, ukimfuata fuata miaka 30 itakuwa inawasubiri, nawaagiza viongozi wote kuanzia kijiji na kata msimamie utekelezaji wa sheria hii ili kumlinda mtoto wa kike," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuwashirikisha wananchi kuwekeza kwenye sekta ya elimu, na kwamba jina la shule hiyo itatambulika kama Shule ya Wasichana Bunge.

"Sote tunakumbuka wabunge wanawake walivyoanzisha mchakato wa fedha kutoka mfukoni na sio za bunge, kazi na michango yote iliyotolewa na wadau zimetumika ipasavyo kama inavyoonekana," alisema.

Alibainisha kuwa ujenzi wa shule hiyo utawezesha watoto wa kike kusoma kwa bidii na kutimiza ndoto zao.

"Nikushukuru Spika kwa maono yako uliyoamua bila kigugumizi, na kuwezesha watoto wa kike kukamilisha elimu yao, niwashukuru wabunge mmechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ujenzi huu," alisema.

Alisema serikali imeweka mikakati ya elimu ya kuwasaidia watoto wa kike kuhakikisha wanasoma kwenye mazingira bora.

Kuhusu majanga ya moto, Majaliwa aliagiza tahadhari za kudhibiti majanga ya moto ziwepo kwenye shule ili kujiepusha na majanga hayo na kutoa elimu kwa wanafunzi namna ya kukabiliana na majanga hayo.

"Shule za serikali ziwe na vifaa vya kudhibiti moto na ukaguzi ufanyike mara kwa mara, na muagize rasmi kwa maandishi ili kuhakikisha shule zote zinakuwa na vifaa vya kuzimia moto sio kwa shule binafsi tu,"alisema.

Waziri Mkuu aliagiza pia Ofisi ya Rais, Tamisemi kuhakikisha katika shule za msingi na sekondari kunakuwa na mwalimu wa kike ili kuwapa uhuru wanafunzi wa kike. Alipongeza Bunge kwa ujenzi wa shule hiyo na kwamba ni Bunge la kwanza Afrika kujenga shule.

Aidha, alitangaza jina la shule hiyo kuwa Shule ya Wasichana ya Bunge (Bunge Girls High School).

Akimkaribisha Waziri Mkuu, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliomba jina la shule hiyo liwe Bunge na lisibadilishwe hata kama majengo yatabadilishwa matumizi kama chuo.



Katibu Mkuu wa Chama cha ADC, Doyo Hassan Doyo (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu msimamo wa chama hicho, kusimamisha wagombea wa nafasi mbalimbali katika uchaguzi mkuu ujao. Kushoto ni Naibu Katibu Mkuu Wanawake, Zuwena Mohamed Abdallah. **PICHA: JUMANNE JUMA**.

# Waliokwama Misri, A. Kusini warejea nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA 57 waliokuwa wamekwama Afrika Kusini kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona wamerejea nchini jana.

Walikwama nchini Afrika Kusini baada ya nchi hiyo kufunga mipaka yake mwanzoni mwa Machi, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilieleza jana kuwa Watanzania hao waliokuwa wamekwama Afrika Kusini kwa takribani miezi mitatu baada ya uwapo wa zuio la kutoka nje waliondoka nchini humo kwa kutumia Shirika la Ndege la Precission Air.

Ilieleza kuwa uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuhusisha Ubalozi wa Tanzania nchini humo ndiyo uliofanikisha kurejea kwa kundi hilo.

Wakizungumza katika Uwanja wa Ndege wa Oliver Tambo, uliopo Afrika Kusini, mmoja wa Watanzania aliyefahamika kwa jina la 'Sunderland the only one' aliishukuru serikali kupitia kwa Balozi wa Tanzania nchini humo, Meja Jenerali mstaafu Gaudence Milanzi kwa kuwa nao pamoja katika kipindi chote ambacho wamekuwa katika zuio nchini humo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa, kundi lingine la Watanzania 38 waliokuwa wamekwama Misri nao walifanikiwa kuondoka nchini humo kwa Shirika la Ndege la Fly Egypt na kuwasili nchini.

Hii ni mara ya pili kwa serikali kufanikisha safari za Watanzania waliokwama ughaibuni, kwamba awali iliwahi kufanikisha safari ya Watanzania waliokuwa wamekwama India.

# Serikali yatoa maelekezo Wiki Utumishi wa Umma

**Na James Mwanamyoto,** DODOMA

SERIKALI imezitaka taasisi za umma nchini kuadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka 2020 kwa kudumisha ushirikiano na wananchi na wadau, ili kuweka mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma bora kwa umma kwa kuzingatia mikataba ya huduma kwa mteja.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika.

Mwanjelwa alisema ushirikiano na wadau ni sehemu ya utekelezaji wa kauli mbiu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka huu ambayo inasisitiza jukumu la utumishi wa umma katika kujenga na kudumisha amani iliyopo miongoni mwa jamii.

"Katika mwendelezo wa kutekeleza kauli mbiu, ninaziagiza taasisi zote za umma kuadhimisha wiki hii kwa kufanya shughuli za kijamii katika maeneo ambayo wananchi wanapata huduma husani kwenye hospitali, masoko na maeneo mengineyo kwa kuzingatia tahadhari dhidi ya corona, kwa lengo la kujenga uhusiano mzuri utakaowezesha utendaji kazi wa taasisi za umma," aliagiza.

Mwanjelwa aliongeza kuwa, watendaji wa taasisi za umma wanatakiwa kuadhimisha wiki hiyo kwa kukutana na watumishi katika maeneo yao ya kazi, ili kusikiliza maoni na vikwazo wanavyokutana navyo katika utekelezaji wa majukumu yao, ikiwa ni pamoja na kukutana na wadau wa nje ili kupata mrejesho wa huduma wanazozitoa, huku tahadhari dhidi ya maambukizo ya corona zikichukuliwa.

Mwanjelwa pia aliwataka watumishi wa umma nchini kutumia maadhimisho hayo kujitathmini kama wanaendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano ambayo imedhamiria kwa dhati kuboresha huduma zitolewazo na taasisi za umma kwa wananchi na hatimaye kuwa na mchango katika maendeleo ya taifa.

Aliziagiza taasisi za umma kuwasilisha taarifa ya namna walivyoshiriki maadhimisho hayo Ofisi ya Rais Utumishi baada ya kilele cha maadhimisho, ili kuiwezesha serikali kutumia taarifa hizo kufanya tathmini na kuboresha utendaji kazi.

Sanjali na hilo, aliwapongeza watumishi wote wa umma kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo licha ya kuwapo kwa tatizo la corona.

# Wabunge wataka watoto wenye ulemavu wa ngozi wasifichwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wamewataka wazazi kuacha kuwaficha watoto wenye ulemavu wa ngozi kwa kuhofia kukatwa viungo au kupoteza maisha wakati wa uchaguzi mkuu, kwa kuwa serikali imejipanga kuhakikisha wanaishi kwa amani.

Rai hiyo waliitoa jizi jijini katika uzinduzi wa kampeni ya 'usiogope tupo pamoja' iliyoandaliwa na Taasisi isiyo ya kiserikali ya Sisi ni Sawa kwa ajili albino.

Walisema hakuna haja ya kuwaficha watoto na kuwazuia kwenda shule kwa kuwa ulinzi juu yao umeimarishwa.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Oliver Semuguruka, alisema hakuna mwanasiasa atakayeshinda kwa kumuua albino wala kwa kumfanya chochote kibaya.

"Wazazi wapelekeni watoto shule, msiogope na wasihi wamama muwapende watoto msiwanyanyapae na wala msiwafiche, hawa ni sawa na sisi," alisema.

Naye, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Mariam Msabaha, alisema wakati wa uchaguzi kumekuwa na maneno kuwa wanasiasa wanaua au kuchukua viungo vya albino kutafutia kura jambo ambalo si sahihi.

"Tusiogope Mungu yupo pamoja nasi, tutashinda, twendeni kwenye uchaguzi pamoja na watoto waende shule tusiogopane na mwenye tatizo tuwasiliane," alisema.

Mbunge wa Same Mashariki (Chadema), Naghenjwa Kaboyoka, alisisitiza watoto wenye ualbino waende kusoma kwa kuwa wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi yeyote kama mtu mwingine wa kawaida.

"Usimfiche mtoto, mtoto atambue na mimi ni binadamu nipo sawa na wengine, na nyie sio walemavu, tutaendelea kushirikiana na serikali mpate misaada ya kila aina," alisema.

Kadhalika, Mbunge wa Mlimba (Chadema), Suzan Kiwanga, aliwataka watoto hao kwenda shule na kuchukua tahadhari kwa kuwa watu wabaya wapo ndani ya jamii.

"Mwamini Mungu nendeni mkasome mchukue tahadhari, watu wabaya wapo ndani yetu iwe wanasiasa au sio wanasiasa, wachimba madini, wewe unamwogopa mwanasiasa kumbe adui yako sio mwanasiasa, kama wapo haiwasaidii," alisema.

Akizindua kampeni hiyo, Balozi wa watu wenye ualbino ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati, alitoa wito kwa taasisi hiyo kuendelea kushirikiana na wabunge ili kutoa elimu ya jamii na kuleta usawa.

Awali, Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, George Kiatika, alisema kumekuwa na dhana kuwa katika kipindi cha uchaguzi albino wamekuwa wakikatwa viungo na wengine kupoteza maisha na imejengeka kuwa wanasiasa wanapoingia kwenye uchaguzi matukio hayo ndio hutokea.

"Hatuamini kama hutokea hivyo ndio maana tumeona tuje na kampeni ili kuelimisha jamii kwamba sisi sote ni sawa, ili kutambua hao ni ndugu zetu na wana uwezo tuwape nafasi ya kushirikiana nao," alisema.

Alisema kampeni hiyo itafika kwenye mikoa 20 nchini huku akiwaomba wabunge kwenye kampeni za uchaguzi kutoa elimu kuwa watu ualbino ni sawa na wengine.

Naye, mratibu wa kampeni hiyo, Henry Mdimu, alisema wenye ulemavu wa ngozi wanapitia kero nyingi na kusababisha kutofikia malengo yao, bila kujua kwamba wana uwezo sawa na wengine.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) mkoani Dar es Salaam wakishiriki kupanda miti katika maeneo ya kuzunguka kiwanda cha bia cha Ilala katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito wafurahia uzinduzi hospitali wilaya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAJAWAZITO wilayani Shinyanga wamefurahia kuzinduliwa kwa hospitali ya wilayani hiyo, ambayo itawaondolea adha ya kufuata huduma zaidi ya kilomita 100 katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo mjini Shinyanga.

Walibainisha hayo kwenye uzinduzi wa hospitali hiyo, ambayo ilianza kujengwa mwaka jana na kukamilika Mei mwaka huu kwa gharama ya shilingi bilioni 1.5.

Baadhi ya wajawazito Elizabeth Paulo na Rejina Wiliam, walisema walikuwa wakipa adha ya kufuata huduma umbali mrefu kwenda Shinyanga Mjini, na kusababisha baadhi kujifungulia njiani, lakini kupatikana kwa hospitali hiyo imekuwa faraja kwao.

Walisema wanaipongeza sana serikali kwa kutujengea hospitali hii ambayo itakuwa msaada hususan kwa wajawazito, ambao walikuwa tukipata tabu sana kufuata huduma ya matibabu mbali.

Naye Mganga Mkuu wa wilaya hiyo, Mameritha Basike, alisema vifo vitokanavyo na uzazi mwaka jana vilikuwa 14, lakini mwaka huu kuanzia Januari hadi Mei hakuna vifo.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliwataka wananchi kuitumia hospitali hiyo kwenda kupata huduma za afya, na kuacha tabia ya kwenda kwa waganga wa kienyeji, pamoja na wajawazito kuacha tabia ya kujifungulia majumbani au kwa wakunga wa jadi, sehemu ambazo siyo salama.

## Wazazi washauriwa miundombinu elimu

**Na Tiganya Vincent,** KALIUA

WAZAZI mkoani Tabora wametakiwa kutenga siku moja katika wiki ya kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya sekta ya elimu katika maeneo yao kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri ya watoto kupata elimu.

Ushauri huo ilitolewa wilayani Kaliua na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, wakati wa ukaguzi wa ujenzi wa miundombinu ya shule iliyojengwa kutokana na nguvu za wanafunzi ambayo itasaidia kupunguza uhaba wa vyumba vya madarasa.

Alisema muundo wa elimu ya kujitegemea unaotumia Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kwa kushirikisha jamii na wanafunzi katika ujenzi wa madarasa, maabara, mabweni na maktaba utasaidia kuboresha kiwango cha elimu kwa wanafunzi kwa kuwa na mazingira rafiki ya upataji elimu.

Mwanri alisema kuanzia sasa mkoa mzima ni lazima utumie mfumo waliotumia Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua wa ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu kwa kushirikisha wanafunzi na jamii ili kupunguza uhaba wa miundombinu hiyo.

## Agizo kwa vyuo vya maendeleo

**Na Francis Godwin,** IRINGA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Iringa, Hapinnes Seneda, ameagiza vyuo vya maendeleo ya jamii mkoani Iringa kuanzisha miradi ya kiubunifu vikiwamo viwanda vidogo ili kuwawezesha wahitimu na jamii inayozunguka vyuo hivyo kutumia ujuzi huo kwa kukuza uchumi wao.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi vitakasa mikono vya kufungwa katika maeneo ya mikusanyiko ya watu katika vijiji vinavyozunguka Chuo cha Maendeleo ya Jamii (CDTI), Rungemba Mufindi, pamoja na vyeti kwa vijana waliobuni vitakasa mikono hivyo ambavyo watumiaji wataweza kunawa mikono pasipo kushika koki , Seneda alisema ubunifu kama huo wa viwanda vidogo vidogo ndio shabaha kuu ya serikali.

Alisema chuo hicho kimeonyesha mfano kwa vyuo vingine katika kutatua changamoto za mkoa wa Iringa kwani pamoja na kuwatumia vijana wasio na kazi katika vijiji vinavyozunguka chuo hicho kwa ajili ya kuwapatia mafunzo ya kujitegemea kwa kuanzisha utengenezaji wa vitakasa mikono vya kisasa bado chuo hicho kimeweza kutatua changamoto ya utapiamlo kwa jamii kwa kuanzisha kilimo cha mboga na matunda.

Mratibu wa kituo cha ubunifu chuoni hapo, Osward Mhema, alisema vifaa hivyo vilivyobuniwa vinaweza kutumiwa na idadi kubwa ya watu katika maeneo ya mikusanyiko.

## HABARI BUNGENI

# Maeneo yote ya migodi kupimwa

**Na Munir Shemwta,** GEITA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, amezitaka halmashauri nchini kupitia idara zake za ardhi kuhakikisha zinapima maeneo yote yenye migodi ili kuondokana na migogoro.

Mabula alisema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na watendaji wa sekta ya ardhi kwenye mkoa wa Geita akiwa katika ziara ya kukagua utendaji wa sekta ya ardhi pamoja na utekelezaji wa miradi inayofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) mkoa humo.

Mabula alisema, mkoa wa Geita una migodi mingi bila kuwa na suala la upimaji na umilikishaji maeneo ya migodi migogoro kwenye maeneo hayo haitaisha kwa kuwa leseni ya uendeshaji shughuli za uchimbaji madini inaonesha umiliki eneo la chini lenye madini.

Aitolea mfano wa mgodi wa madini wa Nyamongo kuwa, umefanikiwa kupima maeneo yake na sasa mgodi huo pamoja na kuwa na haki ya umiliki eneo la chini la madini, lakini mgodi huo unamiliki pia eneo la juu, hivyo kuondokana na migogoro.

Aliwataka watendaji wa sekta ya ardhi katika maeneo yenye migodi kuangalia namna bora ya kuzungumza na wamiliki hao ili kutambua umuhimu na faida ya kupima maeneo yao kwa lengo la kuondokana na mgogoro.

# Raia Burundi hatiani kuishi nchini kinyemela

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi imemuhukumu raia wa Burundi, Nsengiyuma Mathias (25), kulipa faini ya Sh. 500,000 au kutumikia kifungo cha miezi sita gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya kuishi nchini kinyume cha sheria.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Elimo Massawe.

Hakimu Massawe akitoa hukumu katika shauri hilo, namba 47/2020, alisema amesikia maombi yote na kupitia kifungu cha 45 (1) (i) na (2) Sheria ya Uhamiaji namba 542016, alimuhukumu mshtakiwa kulipa faini ya Sh. 500,000 na atakaposhindwa atumikie kifungo cha miezi sita gerezani.

Awali ilidaiwa na Mwanasheria wa Serikali, Emmanuel John kuwa Mathias alikamatwa Juni 06 mwaka huu, na maofisa wa Idara ya Uhamiaji katika nyumba ya kulala wageni iliyopo Manispaa ya Lindi, bila kuwa na kibali kinachomruhusu kuishi nchini.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akisalimiana na maofisa magereza alipotembelea Gereza la Wilaya ya Longwa mkoani Dodoma. Kushoto kwake ni Mkuu wa Gereza hilo, SSP Mgalla Tadeo Yuda. **PICHA: OFISI YA BUNGE**.

# Osha yaagizwa utoaji wa elimu

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Andrew Massawe, ameutaka uongozi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (Osha), kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi, ikiwamo kuelimisha wananchi ili kupunguza ajali na magonjwa yanayoweza kutokea sehemu za kazi.

Alitoa agizo hilo alipotembelea ofisi za Osha kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya kiutendaji ambayo aliyoyatoa kwa viongozi wa taasisi hiyo Januari, mwaka huu.

"Nimefurahi kuona kuwa maagizo yote niliyoyatoa Januari mmeyatekeleza kama tulivyokubaliana, lakini bado tunahitaji kuongeza nguvu zaidi katika kusimamia sheria, kutoa elimu kwa umma, kushughulikia changamoto za wadau wetu kwa haraka zaidi kwa njia ya majadiliano na hivyo kutimiza azma yetu ya kulinda nguvu kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu," alisema Massawe.

Kwa upande wake Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alitoa taarifa ya utekelezaji wa maagizo mbalimbali ambayo yalitolewa na Katibu Mkuu huyo alipotembelea Januari.

Miongoni mwa maagizo yaliyotolewa na Katibu Mkuu na kutekelezwa na menejimenti ya Osha ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usajili na usimamizi wa sehemu za kazi (WIMS), kuanza kutumia mifumo mingine ya serikali, kuanzisha programu mbalimbali endelevu za kuelimisha wananchi na kuboresha tovuti ya taasisi.

Baada ya kupokea taarifa hiyo, Massawe alieleza kuridhishwa kwake na utekelezaji wa maagizo yake na kuwasisitiza viongozi wa Osha kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuboresha zaidi huduma kwa wananchi.

Osha ni taasisi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu ambayo ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi ya mwaka 2003 ambayo inalenga kuboresha mazingira ya kazi hapa nchini.

# Bandari Karema yairidhisha Nemc

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeelezwa kuridhishwa na utekelezaji wa sheria na kanuni za mazingira katika ujenzi wa mradi wa Bandari ya Karema, katika Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 47.6

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema hayo alipotembelea mradi na kukagua hatua mbalimbali za utunzaji wa mazingira katika ujenzi wa bandari, ikiwa ni sehemu ya ziara yake katika Kanda ya Magharibi ya NEMC inayojumuisha mikoa ya Kigoma, Katavi na Rukwa.

"Mradi huu ni moja ya miradi ya kimkakati ya serikali. Hivyo utekelezaji wake unahitaji uangalizi wa karibu hasa katika usimamizi wa mazingira ili utakapokamilika ulete tija iliyokusudiwa," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema bandari itakapokamilika itasaidia kuchochea uchumi wa Mkoa wa Katavi kwa kurahisisha usafirishaji wa mazao ya chakula kwenda nchi jirani ya Jamhuri ya Watu wa Kongo ambako alisema soko la mazao ya chakula ni kubwa.

"Mkoa wa Katavi unazalisha mazao ya chakula na mifugo kwa wingi, hivyo kukamilika kwa bandari hii kutarahisisha usafirishaji na biashara na kwa hiyo kuinua maendeleo wilaya hii na mkoa kwa ujumla," alisema Gwamaka.

Amesema mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Nemc itaendelea kutoa ushirikiano katika mradi huu kupitia ofisi zake za kanda ya magharibi kuhakikisha mradi unakamilika kwa kulingana na kanuni za uhifadhi wa mazingira," alisema.

Ofisa Uhusiano wa Kampuni Xiamen Ongoing Tanzania, Philipo Mwamunyange, alisema mradi unagharamiwa na serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

"Mradi huu utaishi kwa zaidi ya miaka sitini, hivyo kukamilika kwake kutatoa fursa kwa wananchi kunufaika nao kibiashara," alisema Mwamunyange.

NIPASHE JUMATATU JUNI 15, 2020

Nipashe

Spotika



WA5 WAOLISHINDA BALLON D'OR MWAKA AMBAO HAWAKUSTAHILI UK. 12&13



Messi

# TAKWIMU 5 MESSI NI BORA WA WAKATI WOTE

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amekuwa mwanasoka wa kiwango cha juu kabisa kwa kipindi chote hiki cha uchezaji wake na bila shaka ni mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani ambaye soka limemshuhudia.

Kwa sasa anaongoza kwenye safu ya ufungaji mabao kwenye Ligi Kuu Hispania, maarufu La Liga, akiwa na mabao 19, akimwongoza straika wa Real Madrid, Karim Benzema kwa mabao matano zaidi.

Wakati pengine huu unaweza usiwe msimu wake bora zaidi katika miaka ya hivi karibuni, raia huyo wa Argentina anabakia kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu cha Ulaya na yuko kwenye nafasi ya kushinda tuzo ya 7 ndani ya muongo mmoja tu.

Hebu tuangalie takwimu tano ambazo zinathibitisha kwamba, Messi ni mchezaji bora wa wakati wote:

**1- Mabao 25 kila msimu kwa misimu 10**

Katika ligi tano kubwa za Ulaya, washambuliaji wengi wanakuwa kwenye wakati mgumu wa kufunga mabao 20 kwa msimu. Mara chache sana wanakuwa na uwezo wa kumaliza ligi wakiwa wamefunga mabao 25. Hata hivyo, Messi amevuka hapo kwa kipindi chote cha muongo mmoja.

La zaidi ni kwamba ameshafunga mabao 30 katika kila msimu kwa misimu nane katika muongo huo, huku mwaka 2012, alifunga mabao 50. Mpinzani wake mkubwa, Cristiano Ronaldo alikaribia mwaka 2015 wakati alipofunga mabao 48 ya ligi, akikosa mawili kuifikia rekodi ya mpinzani wake.

**2- Mabao 22 LaLiga akitokea benchi**

Siyo jambo la kawaida kwa mashabiki wa Barcelona kumwona Messi akiwa benchi, lakini inapotokea, raia huyo wa Argentina mara kwa mara anathibitisha kwambe yeye ni 'super-sub' wa daraja la juu kabisa duniani.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or amefunga mabao ya ushindi 34 baada ya kuingiza mchezoni akitokea benchi, kitu kinachomfanya kuwa mchezaji mwenye mchango mkubwa zaidi kuliko yoyote pale Barcelona. Katika hayo amefunga mabao 22 kwenye ligi akiwa anatokea benchi.

**3- Mabao 52 ya adhabu ndogo kwa klabu na nchi**

Sio habari kwamba, Messi ni mtu hatari sana wa kupiga mashuti ya adhabu ndogo nje ya 18. Fowadi huyo amefunga mabao ya adhabu ndogo 46 kwa miamba hao wa Katalunya na sita kwa Argentina.

Mpinzani wake, Ronaldo, hajafunga kwa adhabu ndogo tangu alipojiunga na Juventus.

**4- Mchango wa mabao 1,000**


Wiki chake kabla ya soka la Hispania kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Messi alifunga mabao manne kati ya matano dhidi ya Eibar. Hiyo ikamfanya kuwa mchezaji wa kwanza kutoa mchango wa jumla ya mabao 1,000 kwenye LaLiga.

**5- Hat-tricks 41 kwa Barcelona**

Katika mchezo huo dhidi ya Eibar wakati afikisha mchango wa mabao 1,000, Messi alifunga hat-trick yake ya 41 kwa Barcelona. Jambo la kustaajabisha hiyo ilikuwa ni mara ya pili kufunga mabao manne dhidi ya Eibar, ambapo kwa mara ya kwanza aliwafunga msimu wa 2017/18.

## ISIKUPITE

REAL Madrid imefufua upya mchakato wa kumsajili kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante katika majira ya joto na tayari imewasilisha ofa ya pauni milioni 71 ili kumnasa nyota huyo. Vigogo hao wa La Liga walianza kumsaka Mfaransa huyo tangu alipokuwa akiichezea Leicester City.



Extra Time

# WA5 WAOLISHINDA BALLON D'OR MWAKA AMBAO HAWAKUSTAHILI

**LONDON, England**

KWA miaka mingi, majadiliano yale yale yamekuwa yakitawala kuhusu tuzo za Ballon d'Or. Wachezaji wengi wameshinda tuzo ya Ballon d'Or kutokana na viwango vyao walivyovionyesha kwa klabu na nchi zao.

Tuzo za Ballon d'Or zimetawaliwa na wachezaji wawili, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kwa zaidi ya muongo mmoja.

Hata hivyo, kuna wakati tuzo ya Ballon d'Or inaonekana kutolewa kwa mchezaji ambaye hakustahili kwa kipindi hicho na mara nyingi washambuliaji ndio wamekuwa wakiibeba zaidi kuliko walinzi.

Makala hii inakuchambulia wachezaji watano ambao hawakustahili kutwaa Ballon d'Or katika miaka waliyoshinda.

**#5 Luis Figo (2000)**

Luis Figo alitunukiwa Ballon d'Or miezi michache baada ya kuondoka Barcelona kwenda Real Madrid katika moja ya usajili uliozua utata zaidi katika historia ya soka.

Usajili wake wa pauni milioni 37.2 kutoka Katalunya na kwenda kule Castillan uliwagawanya mashabiki na wengine wakadai kwamba ndio sababu ya kushinda tuzo hiyo.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ureno alishinda tuzo hiyo kwa pointi 197, akimshinda Zinedine Zidane, ambaye alipata pointi 181. Alikuwa mchezaji wa kwanza wa Ureno kushinda tuzo hiyo tangu Eusebio mwaka 1965. Wakati aliposhinda Ballon d'Or kama mchezaji wa Los Blancos, ushindi wake ulionekana ulitokana na kile alichokifanya kule Barcelona.

Uhamisho wake kwenda Santiago Bernabeu kipindi cha majira ya joto mwaka 2000 ndio ulikuwa mwanzo wa zama mpya za Galactico zilizoasisiwa na Rais, Florentino Pérez. Lakini wengi waliamini Figo hakufanya mengi kusababisha kupata Ballon d'Or mwaka huo.

Mzaliwa huyo wa Almada alionyesha kiwango cha kuvutia kwenye safu ya kiungo ya Blaugrana. Lakini hakuwasaidia kutetea taji la La Liga wakati walipopoteza kwa Deportivo la Coruna mwishoni mwa msimu wa 1999/2000.

Mwaka huo wengi waliuona ni wa Fernando Redondo, ambaye alikuwa nahodha wa Real Madrid wakati wakitwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya na alistahili kubeba Ballon d'Or.

**#4 Pavel Nedved (2003)**

Pavel Nedved alitwaa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 3003 kutokana na mchango wake muhimu kwa Juventus. Mwaka huo ulishuhudia kibibi kizee hicho cha Turin kikibeba taji la Serie A, Supercoppa Italiana, na kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Jamhuri ya Czech, ambaye alishinda kwa pointi 190 alifuatiwa na Thierry Henry aliyepata pointi 128, huku Paolo Maldini akishika nafasi ya tatu akiwa na pointi 123.

Kiungo huyo mzaliwa wa kule Cheb alifurahia mafanikio mwaka huo, lakini tuzo ya Ballon d'Or wengi waliona aliyestahili ni Henry. Mfaransa huyo alifunga mabao 42 na kutoa pasi za mwisho 26 kwa Arsenal kwa mwaka mzima, takwimu ambazo zilikuwa kubwa zaidi kabla ya ujio wa Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Henry alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Ligi Kuu England na mwaka huo akawasaidia Washika Bunduki hao kutwaa Kombe la FA na kumaliza nafasi ya pili kwenye EPL. Kwa sifa nyingene alifunga bao la ushindi kwa Ufaransa wakati wakishinda Kombe la Shirikisho na alimaliza nafasi ya pili kwenye tuzo za mchezaji bora wa mwaka wa Fifa mwaka 2003. Wengi waliamimi Henry ndiye aliyestahili kubeba Ballon d'Or.

**#3 Lionel Messi (2010)**

Lionel Messi alichukua tuzo hiyo ya Ballon d'Or kwa mara ya pili mfululizo mwaka 2010, ambapo ulikuwa mwaka wa kwanza ambao tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Fifa iliunganishwa na ya Ulaya.

Raia huyo wa Argentina alifunga mabao 60 kwa Barcelona na Argentina. Lakini wengi wanaona kwamba kulikuwa na wachezaji wengine waliostahili kutwaa Ballon d'Or.

Mzaliwa huyo wa jiji la Rosario, alibeba taji la La Liga na hakuwa na kiwango cha kuvutia kwenye Kombe la Dunia akiwa na Argentina, tofauti na wachezaji wenzake, Andres Iniesta aliyeshika nafasi ya pili na Xavi Hernandez nafasi ya tatu. Zaidi ni kwamba uamuzi wa kutomjumuisha Wesley Sneijder katika tatu bora ya Ballon d'Or kulizua minong'ono katika jamii ya soka.

Iniesta na Xavi walishinda kila kitu sawa na Messi pale Barcelona, lakini walifanya makubwa kule Afrika Kusini, ambapo waliiwezesha Hispania kubeba taji lake la kwanza la Kombe la Dunia. Wawili hao walitawala safu ya kiungo kwa timu ya taifa.

Wakati huo huo, Sneijder alikuwa katika kilele cha mafanikio katika klabu yake ya Inter Milan wakati wakishinda mataji matatu chini ya kocha, Jose Mourinho. Pia alikuwa anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alionyesha kiwango cha juu kwenye michuano ya Kombe la Dunia, wakati alipofunga mabao matano, na kuipeleka fainali Uholanzi kwenye mashindano hayo.

Sneijder pia alitwaa tuzo ya mpira wa fedha na kiatu cha dhahabu kwenye Kombe la Dunia. Mchango wa Mholanzi huyo kwa klabu yake na nchi yake mwaka 2010 ulitosha kumfanya awe kwenye jukwaa la tuzo za Ballon d'Or.

**#2 Cristiano Ronaldo (2013)**

Cristiano Ronaldo alivunja umwamba wa Lionel Messi na kubeba Ballon d'Or mwaka 2013 kwa mara ya kwanza baada ya kujiunga na Real Madrid. Raia huyo wa Ureno hakushinda taji lolote mwaka huo lakini alifunga mabao 69 na kutoa pasi za mwisho 17 kwa klabu na nchi yake.

Na kwa uhakika kabisa kulikuwa na mchezaji mmoja nje ya Lionel Messi, ambaye alipaswa kutwaa tuzo hiyo mwaka huo. Na huyo alikuwa ni kiungo wa Bayern Munich, Franck Ribery, ambaye alimaliza nafasi ya tatu kwenye jukwaa la Ballon d'Or nyuma ya Messi.

Wakati nyota wa Barcelona alifunga mabao 42 kwa klabu na nchi yake licha ya majeruhi, Ribery alikuwa nguzo ya mafanikio kwa Bavaria wakati wakishinda mataji matatu na wengi waliamini yeye ndiye alistahili kushinda tuzo hiyo mwaka 2013.

Ribery alifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 18 katika mashindano yote, akabeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Bayern Munich, akashinda Bundesliga, Kombe la Ujerumani, UEFA Super na Klabu Bingwa ya Dunia.

**#1 Luka Modric (2018)**

Wakati Luka Modric aliposhinda Ballon d'Or mwaka 2018, alikuwa mchezaji wa kwanza kutoka nje ya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kuibeba tuzo hiyo tangu Kaka mwaka 2007.

Kiungo huyo wa Real Madrid alitwaa Ballon d'Or kutokana na mchango wake kwa miamba hao wa Hispania kwa kushinda mara tatu mfulilizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na mchango wake wa Croatia kutinga fainali ya Kombe la Dunia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 alipata pointi 753, akifuatiwa na Cristiano Ronaldo aliyepata pointi 476 na Antoine Griezmann akiwa na pointi 414. Lionel Messi, ambaye alikuwa katika tatu bora ya Ballon d'Or kila mwaka tangu 2006, hakuwapo jukwaa kwani alishika nafasi ya tano akipata pointi 280. Huku Kylian Mbappe akimaliza nafasi ya nne juu ya Messi na kupata pointi 347.

Jamii ya soka ilionekana kutoridhishwa na mshindi wa tuzo hiyo ya Ballon d'Or, ambaye alifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho 11 kwa klabu na nchi yake.

Wengi waliamini kwamba, tuzo hiyo alistahili Messi ambaye alifunga mabao 51 kwa Barcelona na kutoa pasi za mwisho 26 katika mechi 54 alizocheza kwenye mashindano yote kwa klabu na nchini yake na alitawala kwenye takwimu za La Liga.


Alishinda taji la ligi na Copa del Rey mwaka huo. Lakini kutofanya vizuri kwenye Kombe la Dunia na kushindwa kutamba kwa Blaugrana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, inaaminika ndio sababu ya kushindwa kubeba Ballon d'Or dhidi ya Modric mwaka huo.



Luka Modric

## Nukuu

"Nafikiri kwa hali yangu binafsi, hii imekuwa likizo ndefu zaidi kwangu, nimekuwa na wakati wa kupumzika. Nafikiri ni zaidi ya miaka mitano iliyopita ndio safari hii nimepata muda wa kupumzika ni muda mrefu zaidi kiakili na kimwili. Nilikuwa na wakati wa kupumzika na familia yangu, watoto wangu na sasa nipo tayari kwa ajili ya mapambano." **Mshambuliaji wa Antoine Griezmann alisema akizungumza na Barca TV.**



"Salah alipokuja Chelsea, alikuwa kijana mdogo, alikuwa mtulivu sana na kila mtu alimpenda, sikuwahi kufikiria kabisa angefikia kiwango hiki alichonacho kwa sasa, naona maajabu makubwa kwa kweli," **alisema John Obi Mikel alipokuwa akizungumza na Sky Sport.**



"Barcelona mara zote wamekuwa wakinunua wachezaji wakubwa. Binafsi sina uhakika kama Suarez anahitaji mrithi wake, naamini Griezmann (Antoinne), ataimarika," **Arsene Wenger alisema hayo alipozungumza na BeIN SPORTS.**





# REKODI 5 KALI ZA LIGI KUU BAADA YA CORONA

Golikipa wa Mwadui FC, Mohamed Amir, akidaka moja ya mashuti yaliyopigwa langoni mwake na wachezaji wa Yanga, huku kiungo Patrick Sibomana akinyemelea kuangalia kama mpira unaweza kumponyoka. **PICHA: MTANDAO**

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2019/20, zimerejea tena baada ya kusimama kwa zaidi ya miezi miwili kutokana na janga la ugonjwa wa corona (COVID-19).

Mechi zilizofungua dimba zilichezwa Jumamosi kati ya Mwadui iliyoikaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Kambarage mkoani Shinyanga na kushuhudia wenyeji wakianguka kwa kuchapwa bao 1-0.

Mechi nyingine ilipigwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Coastal Union ilipokuwa nyumbani kupepetana na Namungo na mechi kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Hizi ndizo mechi zilizoweka rekodi ya kuwa za kwanza za Ligi Kuu kuchezwa baada ya serikali kuruhusu michezo kuanzia Juni Mosi, mwaka huu baada ya kupiga marufuku ili kupambana na ugonjwa huo tangu Machi 17, mwaka huu.

Lakini pia ni mechi za kwanza nchini kuchezwa kukiwa na kanuni mpya ambazo mbali na zile za kiafya, pia za kubadilisha wachezaji kutoka watatu hadi watano.

Zifuatazo ni baadhi ya rekodi zilizowekwa kwenye mechi hizo mbili za kwanza baada ya mapumziko kupisha janga la corona, kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga na Mkwakwani Tanga.

**1. Yanga ya kwanza kushinda**

Yanga imekuwa timu ya kwanza kushinda baada ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuruhusiwa kuendelea.

Ushindi wa bao 1-0 ilioupata dhidi ya Mwadui umeifanya timu hiyo kuingia kwenye rekodi hiyo, huku timu tatu zilizobaki zilizocheza mechi za ufunguzi baada ya ruhusa kushindwa kufanya hivyo.

Mwadui imefungwa, huku mechi ya Coastal Union na Namungo zikishindwa kuweka rekodi hiyo kwa kutoka sare ya magoli 2-2.

**2. Mwadui FC ya kwanza kufungwa**

Timu ya Mwadui nayo imeingia kwenye rekodi ya kuwa timu ya kwanza kupoteza mechi baada ya Ligi Kuu kusimamishwa kwa ajili ya corona.

Kipigo cha nyumbani cha bao 1-0 dhidi ya Yanga kwenye moja kati ya mechi mbili za kwanza, kinawafanya kuweka rekodi hiyo mbaya, ikizingatiwa timu nyingine zilizocheza siku hiyo, Coastal Union na Namungo FC zimetoka sare ya magoli 2-2.

3. Makang'a amfunika Mapinduzi

Wakati mashabiki wengi nchini wakiamini kuwa kiungo wa Yanga, Mapinduzi Balama ndiye atakuwa mchezaji wa kwanza kufunga goli baada ya mapumziko ya corona kutokana na kufunga bao hilo mapema tu dakika ya tano, mama si kama yalivyo.

Rekodi hiyo imeenda kwa mchezaji wa Namungo, George Makang'a ambaye yeye amefunga goli kwenye dakika ya tatu ya mchezo dhidi ya Coastal Union.

Mabao mengine yalifungwa na Abeid Athumani dakika ya 17, huku Coastal Union wakisawazisha kupitia kwa Issa Said dakika ya 53 na Hance Rashid dakika ya 59.

**4. Molinga kuingia dakika za majeruhi**

Straika tegemeo wa Yanga, David Molinga yeye ameweka rekodi ya kuingia uwanjani ndani ya dakika tatu za majeruhi zilizoonyeshwa na mwamuzi wa akiba.

Baada ya kuonyeshwa dakika tatu, mechi ilichezwa kama dakika mbili hivi, ikabaki moja ndipo Molinga alipoingia akichukua nafasi ya Ditram Nchimbi.

Mkongomani huyo aliyesafiri kwa ndege baada ya kugoma kuondoka na mwenzake, alikwenda Shinyanga akiongozana na Kocha Mkuu, Luc Eymael na dakika moja tu ilimtosha kufanya kazi aliyotakiwa kuifanya uwanjani.

Ilionekana kabisa kuwa aliingia kwa kazi ya kupoteza muda, na kweli alirushiwa mpira na kuanza kusukumana na mabeki wa Mwadui, akiwazuia wasichukua mpira ili dakika hiyo moja imalizike na alifanikiwa.

Molinga ndiye straika anayeongoza kwa magoli kwenye kikosi hicho akiwa amefunga magoli nane.

**5. Ni Wabongo tu wametupia**

Kwenye mechi mbili za ufunguzi baada ya corona, mabao matano yamefungwa na yote yakifungwa na wachezaji Watanzania tu.

Hii ina maana Wabongo watupu wameweka rekodi ya kufunga magoli yote ya mechi za mwanzo baada ya mapumziko kupisha corona.

Wachezaji hao ni pamoja na Balama wa Yanga, Makang'a, Athumani Abeid wa Namungo, Issa Said na Hance Rashid wa Coastal Union.

Kwenye timu hizo nne zilizocheza mechi za kwanza baada ya mapumziko, timu za Coastal Union na Mwadui FC hazina wachezaji wa kigeni, huku Yanga na Namungo zikiwa na baadhi ya wachezaji kutoka nje ya nchi.

**JE, WAJUA?**



SIPHIWE Tshabalala ndiye alifunga bao katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya Kombe la Dunia dhidi ya Mexico ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1. Mechi hiyo ilichezwa Juni 11, 2010.



## HABARI DODOMA

# Kidato cha 6 wapewa siri ufaulu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WANAFUNZI wa kidato cha sita wanaotarajiwa kufanya mitihani yao Juni 29, mwaka huu, wametakiwa kujiandaa vyema ili kupata ufaulu mzuri kwenye masomo yao.

Wito huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Dodoma, Winifrida Kaliyo, alipokuwa akikabidhi misaada ya vifaa mbalimbali kwenye Kituo cha Afya cha Mkonze na Shule ya Wasichana ya Sekondari Msalato vyenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Vifaa hivyo pamoja na mashuka 50 kwa ajili ya kituo hicho ambacho kilikuwa kinatumika kuhudumia wagonjwa wa corona na vifaa vya kufanyia mitihani kwa wanafunzi wa kidato cha sita wa shule hiyo.

Akikabidhi misaada hiyo, Mwenyekiti huyo, aliwahimiza wanafunzi wafanye vizuri katika mitihani yao kwa kuwa ni viongozi watarajiwa.

"Jumuiya yetu inawatambua nyinyi kama viongozi wa sasa, jitihada zenu ndizo zitakazowafikisha mahali ambapo mnahitaji kufika, na imani mmejiandaa vyema kwa mitihani yenu ya mwisho na niwatie shime watoto wangu mfanye vizuri kwenye mitihani hiyo ili wote mpate daraja la kwanza," alisema.

Aliwataka kutokuwa na hofu katika mitihani hiyo bali wamtangulize Mungu na yeye atakuwa msaada wa kukumbuka kila walichofundishwa.

Naye, Katibu wa UWT wa Wilaya hiyo, Diana Madukwa, alisema juhudi kubwa zinazofanywa na Rais John Magufuli zimekuwa chachu ya kuwasukuma na kuona kuwa na wao wanapaswa kumuunga mkono.

"Nchi yetu ilipita katika kipindi kigumu cha mapambano ya corona na wenyewe mlijionea jinsi Rais wetu alivyosimama imara kwenye misimamo bila ya kuyumbishwa, misimamo yake na kwa uwezo wa Mungu akatuvusha, hivyo sisi wanawake tukaona namna bora ya kufikisha pongezi na shukrani zetu ni kusaidia kutoa utoaji wa huduma katika sekta ya afya," alisema katibu huyo.

# Bilioni 96/- zawekezwa sekta ya kilimo miaka 4

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, amesema katika kipindi cha miaka minne serikali imewekeza Sh. bilioni 96, katika sekta ya kilimo cha umwagiliaji nchini.

Hata hivyo, amesisitiza miradi yote ya umwagiliaji nchini kuendeshwa kibiashara ili kurudisha mitaji na kupanua uwekezaji.

Mgumba, aliyasema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na viongozi pamoja na wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NIRC).

Alisema ni wakati sasa miradi yote ya umwagiliaji nchini, kuanza kuendeshwa kibiashara ili kurudisha mitaji mikubwa iliyowekezwa na serikali na kupanua eneo la uwekezaji huo katika sekta hiyo nchini.

Alisema miradi hiyo ndiyo ambayo imebakia kuwa sehemu ya serikali kuwekeza fedha bila kupata mapato, hivyo sasa ni lazima Tume hiyo kuona namna ya kuendesha miradi hiyo kibiashara.

"Miradi hii inatumia fedha nyingi sana za uwekezaji kutoka serikali kuliko miradi mingine, lakini hakuna kiasi chochote ambacho serikali inakipata kwa hivi sasa, ukiangalia hata kwenye miradi ya vituo vya afya pamoja na kuwa ni ya jamii, lakini watu wanachingia, kumwona daktari tuu ni Sh. 8,000 au 10,000," alisema Mgumba.

Alisema bila miradi hiyo kuendeshwa kibiashara mtiririko wa ukuaji wa sekta hiyo utayumba.

"Kama mradi tumewekeza bilioni tatu, tukipata faidi basi tutakwenda kuwekeza katika maeneo mengine ili kuwa na kilimo cha uhakika ambacho hakitegemei maji ya mvua kwa asilimia 100, na kuongeza uchumi wetu, kuongeza pato la taifa pamoja na kuwa na uhakika wa chakula ili kumpiga adui umaskini," alisema Mgumba.

Aidha, alisema ni lazima miradi yote ya umwagiliaji ambayo serikali imewekeza kukusanya mapato angalau kwa asilimia tano ya mapato kwani mpaka sasa hakuna kilicho kusanywa.

Mgumba alisema kabla ya mwezi Julai mwaka huu, lazima kuwe na mfuko wa umwagiliaji pamoja na mwongozo wake utakaosaidia katika uboresha sekta hiyo.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Daudi Kaali, alisema Tanzania ina hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo hicho.

"Kati ya hekta hizo, hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, hekta milioni 4.8 zinauwezekano wa kati na ketka milioni 22.3 zinauwezekano mdogo wa kumwagiliwa," alisema Kaali.

Alisema hadi kufikia mwaka 2015, kabla ya kuanza kwa tume hiyo, jumla ya hekta 461,000 zilikuwa zimeendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji.



Vijana kutoka kundi la watu wenye ulemavu wa ngozi wakiosha magari ikiwa ni sehemu ya Siku ya Maadhimisho ya Kimataifa ya Kuongeza Uelewa kuhusu Ualbino yalifanyika jana, jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA** .

# Mpango aipongeza benki ahueni urejeshaji mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imeagiza benki na taasisi za fedha kutathmini kwa kina athari zinazotokana na mlipuko wa Covid-19 kwenye urejeshaji wa mikopo ya wateja wa taasisi hizo.

Imeipongeza benki ya Exim Tanzania kwa kuongeza muda wa urejeshaji wa mikopo ili kusaidia wateja wa benki hiyo ambao biashara zao zimeathiriwa zaidi na janga hilo.

Akiwasilisha bungeni mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/21 jijini Dodoma wiki uliiyopita, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, mbali na kuipongeza benki hiyo alitoa wito kwa benki nyingine nchini kujadiliana na kukubaliana na wakopaji namna ya kurejesha mikopo na kutoa unafuu wa urejeshaji wa mikopo.

"Serikali kupitia Benki Kuu itatoa unafuu kwa benki na taasisi za fedha zitakazotoa unafuu katika urejeshwaji wa mikopo hiyo kwa kuzingatia uwazi na bila upendeleo. Katika hili, napenda kuzipongeza baadhi ya benki kama Exim ambazo tayari zimetangaza kuongeza muda wa urejeshaji wa mikopo, ili kusaidia wateja wao katika sekta ambazo biashara zao zimeathiriwa na Covid-19 na naziomba benki nyingine zifuate mfano huo," alisema.

Katika kukabiliana na athari za janga hilo serikali ilichukua hatua kadhaa ili kunusuru uchumi ikiwamo kushusha kiwango cha riba kinachotozwa kwa benki kukopa Benki Kuu kutoka asilimia 7 hadi asilimia 5 hatua ambayo ililenga kuongeza wigo wa benki kukopa kutoka Benki Kuu kwa riba nafuu ili nazo ziwezi kupunguza riba ya mikopo kwa wateja.

Kauli hiyo ya Waziri Mpango imekuja siku chache kufuatia Benki ya Exim kutangaza msamaha wa likizo ya malipo ya mikopo kwa wateja wake wakubwa, wa kati na wadogo walipo katika sekta zilizoathirika zaidi kiuchumi kutokana na athari za mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona (COVID -19).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki hiyo hivi karibuni ikimnukuu Ofisa Mtendaji Mkuu, Jaffari Matundu, msamaha huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 160 ulianza Juni mwaka huu, ukihusisha likizo ya malipo ya mikopo kwa wateja na nyongeza ya muda wa urejeshaji wa mikopo ili kusaidia wateja wa benki hiyo katika sekta mbalimbali kutokana na athari za janga hilo kwenye biashara zao.

Alisema msamaha huo unazingatia vigezo mbalimbali kwa kila mteja kwa kuwa athari za Covid-19 hazikuwa sawa katika sekta zote. "Tunafarijika kwa kuwa tayari wateja waliopo kwenye sekta zilizoathiriwa zaidi wameshaanza kusaidiwa. Mazungumzo na wateja wengine bado yanaendelea ili kutambua hatua mbalimbali zinazofaa kulingana na aina ya biashara," aliongeza.

Akizungumzia uamuzi wa benki hiyo Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Peter Kifunguomali, alisema kuwa utasaidia wafanyabiashara wengi zikiwamo kampuni hususani zinazohusika na sekta zilizoathirika zaidi ikiwemo sekta ya utalii kuweza kupata muda wa kutosha kujiimarisha tena kibiashara ili yaweze kupata nguvu ya kurejesha mikopo hiyo bila kutetereka.

"Ukweli ni kwamba athari za corona zimeathiri kwa kiasi kikubwa sekta muhimu na wafanyabiashara wengi kwa sasa wanaumiza namna ya kujinasua na janga hili. Uamuzi uliofanywa na benki ya Exim unapaswa kufanywa na benki nyingine pia ili kunusuru wateja wao ambao kimsingi kwasasa wanahitaji msaada ambao naamini benki zinaweza kuwasaidia," alisema. alisema.

HABARI MBEYA

# Madiwani wamaliza kazi kwa azimio

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, limehitisha shughuli zake kwa kutoa azimio la kufukuzwa kazi mtumishi mmoja wa halmashauri hiyo ambaye amehukumiwa kwenda jela miaka miwili baada ya kukutwa na hatia ya kufanya uzembe na kusababisha mtu kuzikwa akiwa hai kwenye eneo lake la utawala.

Kikao cha mwisho cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya hiyo, kiliketa mwishoni mwa wiki mjini Rujewa na kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo, lakini baadaye kilijigeuza kuwa kamati ya kujadili nidhamu na mwenendo wa watumishi wake na ndipo baraza hilo likatoa azimio kuhusu mtendaji wa Kijiji, Nelson Lupakisyo.

Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Uswege Kaminyoge, alisema walifikia uamuzi huo baada ya Akizungumzia uamuzi huo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Brown Mwakibete, alisema azimio hilo limetolewa kwa kuzingatia sheria za nchi, na kwamba ikiwa mtumishi huyo atakata rufani mahakamani na kushinda, baraza hilo linaweza kutoa maamuzi mengine kulingana na matakwa ya sheria.

Kwa mujibu wa Mwakibete, Sheria za Utumishi wa Umma, Lupakisyo ana nafasi ya kukata rufani na kama atashinda baraza linaweza kufanya uamuzi mwingine.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo, Kivuma Msangi, alisema mtumishi huyo kabla ya uamuzi huo alikuwa akiendelea kupata stahiki zake zote mpaka alipohukumiwa na mahakama.

"Kulitokea mauaji katika eneo lake la utawala, mtu alizikwa akiwa hai kwenye upelelezi ilibainika kuwa alifanya uzembe, hivyo alifunguliwa kesi tangu mwaka 2015, huku akiwa mahabusu baada ya mahakama kutoa uamuzi alitakiwa kwenda jela miaka miwili...kutokana na hali hiyo halmashauri inatulazimu tumfukuze kazi," alisema Msangi.

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, limehitimishwa rasmi kwa kikao hicho na sasa linasubiriwa tamko la waziri mwenye dhamana kwa ajili ya kuvunjwa ili kupisha uchaguzi mkuu wa madiwani, wabunge na urais unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.



Mkurugenzi wa kituo cha watoto yatima cha Nuru kilichopo eneo la Igawilo jijini Mbeya (wa pili kushoto), Jason Fihavango, akipokea msaada wa vitu mbalimbali mchele, maharage, juisi, mafuta ya kupikia na kupakaa vilivyotolewa na Kampuni ya Qnet inayojihusisha na usambazaji bidhaa kwa njia ya mtandao, wengine kushoto ni kiongozi wa msafara, Erneus Mwandoloma na Meneja Miradi wa Kituo cha Nuru, Osward Poyo. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Wataka kituo cha afya kwa mabango

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANANCHI wa Kijiji cha Ifupa, kilichopo wilayani Mbeya wameandamana huku wakibeba mabango kwa lengo la kuomba serikali iwasaidie shughuli za ujenzi wa kituo cha afya cha kata ya Ilungu ambacho wameanza kujijenga kwa nguvu zao, ili waweze kuondokana na adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya.

Mbali na maandamano hayo wananchi hao pia walijitolea kuuza mali zao mbalimbali na kisha kufanya harambee ya kuchangishana kwa lengo la kupata fedha za kuendelea na ujenzi wa kituo hicho.

Wakizungumza wakati wa tukio hilo, baadhi ya wananchi hao walisema wanalazimika kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya kwenye Hospitali Teule ya Wilaya iitwayo Ifisi iliyopo katika mji mdogo wa Mbalizi ambako ni umbali wa zaidi ya kilometa 70 kutoka kijijini hapo.

Tumain Yusufu alisema kuwa wamekuwa wakisikia tu kwenye vyombo vya habari kwamba serikali ya awamu tano inajenga vituo vya afya na hospitali za wilaya kwenye maeneo mengine nchini, jambo ambalo wao wanadhani ni miujiza kwasababu halijawahi kutokea kwenye kata yao.

"Tumesikia kuwa Rais Magufuli anajenga vituo vya afya na hospitali nyingi nchini, lakini sisi tunadhani hiyo ni miujiza tu, maana haijatokea hapa kwetu, tunaomba kama kweli hayo yanafanyika nasi atukumbuke kwenye kituo chetu hiki ambacho tunajenga kwa nguvu zetu ili nasi tuione miujiza hiyo," alisema Tumaini.

Alisema kuwa wananchi wa Kata ya Ilungu hasa wajawazito na watoto wanapata shida kubwa ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za afya kama vile upasuaji na magonjwa mengine yasiyoweza kutibika kwenye zahanati ya kijiji kwa kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 70 kwenda kwenye Hospitali Teule ya Wilaya.

Katibu wa kamati ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ifupa, Zacharia Noti alisema tangu waanze ujenzi wa kituo hicho cha afya mwaka 2017 chanzo kikuu cha mapato kwa ajili ya ujenzi ni michango ya wananchi pamoja na misaada ya wadau wachache wa maendeleo.

Alisema wananchi hao wamekuwa wakifanya harambee ya kuchangishana fedha kila Ijumaa, ambapo mpaka sasa walishafanya harambee 76 na kufanikiwa kupata zaidi ya Sh. milioni 98.

"Tunachangishana kila siku ya Ijumaa na mpaka sasa tumeshafanya harambee 76 za kukusanya fedha za ujenzi. Kutokana na harambee hizo, tumeshafanikiwa kukusanya zaidi ya shilingi milioni 98 ambazo zote tunazielekeza kwenye ujenzi wa kituo chetu cha afya," alisema Noti.

Alisema wadau wachache ndio ambao waliwahi kuwasaidia fedha za ujenzi ambao ni pamoja na aliyekuwa Mwenyekiti wa IPP, Hayati Dk. Reginald Mengi, aliyewachangia shilingi milioni 25, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oren Njeza aliyewachangia mifuko 200 ya saruji pamoja na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa) iliwasaidia kukamilisha ujenzi wa nyumba ya mganga ambayo wananchi walikuwa wameshaijenga mpaka kufikia hatua ya mtamba wa panya.

Alisema mpaka kwa msaada huo wa wadau pamoja na nguvu za wananchi, wamekamilisha ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD), nyumba ya mganga na choo, huku jengo la mama na mtoto likiwa kwenye hatua ya kupaua na jengo la upasuaji ambalo wameanza kujenga msingi.

Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Ifupa ambaye ndiye Mganga Mfawidhi wa Zahati ya Kijiji hicho, Bahati Mongita, alisema wananchi hao tayari wameshaanza kuchukua hatua dhidi ya changamoto zao za kiafya na wanachohitaji ni kuungwa mkono na serikali.

# Watoto wenye uhitaji wasaidiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KAMPUNI ya Qnet inayojishughulisha na uuzaji wa bidhaa vikiwamo vifaa tiba na vidani kwa njia ya mtandao imetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa ajili ya kukisaidia kituo cha kulelea watoto yatima cha Nuru kilichopo eneo la Igawilo, jijini hapa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo, kiongozi wa msafara, Erneus Mwandoloma, alisema umegharimu shilingi milioni moja na kwamba vitu vilivyotolewa ni pamoja na maharage, mchele, mafuta ya kula na kupakaa, juisi na pampasi za watoto.

Mwandoloma alisema kampuni hiyo imekuwa na utaratibu wa kuwasaidia wenye mahitaji na kwamba kwa Mkoa wa Mbeya ni mara ya kwanza na kuahidi kukitembelea kituo hicho mara kwa mara pamoja na maeneo mengine.

"Ni mwaka sasa tangu tuanzishe kampuni yetu hapa mbeya licha ya kuwa tayari mikoa 12 inanufaika na huduma yetu, mbali na kuuza bidhaa zetu kwa njia ya mtandao lakini tunajitahidi kurudisha fadhili kwa jamii yetu inayotuzunguka kwa kuwapatia misaada, tumeguswa na mahitaji ya kituo hiki ndio maana tumeamua kuwatembelea watoto hawa ambao hawakutamani kufiwa na wazazi au kutokea kwa matatizo katika familia zao tunaahidi tutakuwa tukiwatembelea," alisema Mwandoloma.

Meneja miradi wa kituo hicho, Osward Poyo, alisema wanahudumia watoto 26 na kati yao wakike ni 12 na wakiume ni 14, akiwamo wenye umri wa miezi tisa.

Alisema kituo hicho kinapokea watoto kutoka Jeshi la Polisi kitengo cha Dawati la Jinsia na Ustawi wa Jamii na kwamba miongoni mwa sababu zinazosababisha watoto hao kupelekwa hapo ni mzazi kufariki wakati wa kujifungua, wazazi wenye matatizo ya akili na migogoro ya familia.

"Kituo hiki kilianzishwa mwaka 1998 hadi sasa tumewalea watoto 190 ambao wengine sasa wako vyuo vikuu, tunajivua kuwa sehemu ya mafanikio yao maana tunajitahidi kwa kushirikiana na nyie wadau wetu kuwalea watoto hawa," alisema Poyo.

Mkurugenzi wa Kituo Nuru, Jason Fihavango, aliishukuru kampuni hiyo kwa msaada walioutoa na kuwaomba kuendelea kuwatembelea mara kwa mara ili watoto hao waendelee kupata faraja.

Aliongeza kuwa jamii inayowazunguka sasa imeanza kuwatamani watoto hao baada ya kuona wadau mbalimbali wanafika hapo kuwatembelea na kuwapatia misaada mbalimbali alisema awali watoto hao walikuwa wakinyanyapaliwa kutokana na hali zao.





# CCM yatangaza fomu kinyang'anyiro urais

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar kimetangaza rasmi kwa wanachama wa chama hicho, wanaotaka kugombea nafasi ya urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu kuanza kuchukua fomu.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Ofisi Kuu za CCM Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Abdallla, Juma Saadalla, alisema fomu za kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar zitatolewa kuanzia leo Juni 15 hadi 30 mwaka huu.

Alisema kuwa mwanachama anayetaka kuwania nafasi hiyo, atalazimika kuchukuwa fomu na kuijaza kwa kupata wadhamini 250 katika mikoa isiyozidi mitatu ya Zanzibar.

Alisema itapendeza zaidi wagombea hao wakipata wadhamini kutoka katika mkoa mmoja wa Unguja na mwingine wa Pemba, huku wadhamini hao wasiwe wajumbe wa Kamati Kuu au Halmashauri Kuu ya (NEC).

Dk. Sadalla alisema wanachama wa CCM watakaochukuwa fomu kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar watalazimika pia kuzifahamu kikamilifu kanuni za viongozi pamoja na katiba ya CCM na maadili ya chama kwa viongozi.

"Hayo ndiyo mambo muhimu kwa viongozi kuyafahamu wakati wanapotaka kuwania nafasi kubwa ya juu ya uongozi wa urais wa Zanzibar... katiba ya chama waifahamu kikamilifu pamoja na maadili ya viongozi na kanuni za viongozi pia," alisema.

Alieleza kuwa mambo ambao hayatakiwi kwa waanachama wanaokwenda kuchukua fomu za urais wa Zanzibar ikiwamo shangwe na vificho pamoja na misafara ya magari.

"Chama chetu kimekataza kabisa watu wenye nia kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar kuja hapa na misafara ya magari na shangwe na vigelegele... wanatakiwa kuja na watu wao, ambao wanaweza kupiga picha za kumbukumbu hilo ni jambo la kawaida," alisema Sadalla.

Filimbi ya kuchukuwa fomu za urais wa Zanzibar inakuja kufuatilia Rais aliopo madarakani Dk. Ali Mohamed Shein kumaliza muda wake wa uongozi wa miaka kumi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano.



Baadhi ya wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa-Zanzibar), wakiwa katika mkutano mkuu wa chama hicho Tunguu mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Tamwa yawaondoa hofu wanawake kuwania uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa-Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, alisema pamoja na kazi kubwa wanayoifanya katika kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi, lakini bado nafasi hizo hazijatumiwa ipasavyo ili kufikia lengo.

Akizungumza na wanachama wa Tamwa katika mkutano mkuu wa chama hicho, Tunguu, alisema miongoni mwa vikwazo vinavyosababisha kutofikia lengo hilo ni kutokujiamini na kukatishwa tamaa mapema.

Alisema ni vyema wanawake kutambua kuwa wana haki ya kufanya hivyo, kutokana na kuwa wanaweza kuwatumikia wananchi kutokana na kuwa karibu zaidi na wanajamii na kufahamu masuala ya kuyafanyia kazi.

Dk. Mzuri aliwataka wanawake wakiwamo wanachama wa Tamwa kutumia fursa ya kugombea nafasi mbalimbali ikiwamo; Uwakilishi na Ubunge ili kufikia asilimia 50 pasipo kuhofia vitisho vya wanaume.

"Huu ni mwaka wa uchaguzi, hivyo wanawake lazima kujipanga na kuhakikisha huu ni mwaka wetu tunajitokeza kwa wingi kugombea nafasi za uongozi majimboni na kuhakikisha nafasi hizo tunashinda."

Aidha, aliwataka wanawake kutojilemaza na nafasi za viti maalum katika nafasi za uwakilishi na ubunge na badala yake nafasi hizo ziwe ni njia za kuelekea jimboni kugombea nafasi za uongozi.

Kwa upande wao washiriki wa mkutano huo walisema kumekuwa na tabia kwa viongozi wanaobahatika kuchaguliwa kujimilikisha majimbo hayo, ili kuwawekea vikwazo wanawake wanaotaka kugombea hivyo wanapaswa kufahamu kuwa kila mmoja ana haki ya kugombea na kuchaguliwa.

"Wapo baadhi ya wabunge na wawakilishi majimboni wapo zaidi ya miaka 20 na kujimilikisha majimbo hayo kuwa ni yao, hali ambayo inawafanya wanawake wanaotaka kugombea kukosa nafasi," alisema Kauthar Is-haka mwanachama wa Tamwa.

Mkutano huo wa siku mbili uliowashirikisha wanachama wa Tamwa umejadili ajenda mbalimbali ikiwamo mpango mkakati wa chama kwa miaka mitano ijayo ripoti ya fedha pamoja ripoti ya utendaji wa mwaka.

## ZEC yajizolea sifa vitambulisho kura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar itawapatia vitambulisho vipya wapigakura wote walioandikishwa na kuhakikiwa taarifa zao katika daftari la kudumu la wapigakura ambavyo vitawawezesha kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Mkurugenzi wa Uchaguzi Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Thabati Idarous Faina, alisema hayo baada ya kutembelea vituo vya uandikishaji vya wilaya ya mjini kwa lengo la kuangalia mwenendo wa utoaji huduma kwa wananchi wanaofika vituoni kwa ajili ya kuandikishwa na kuhakikiwa taarifa zao.

Mkurugenzi huyo, alisema kukamilika kwa zoezi la uandikishaji kwa mara ya pili ni hatua ambayo itaifanya Tume kuweka wazi daftari la kudumu la wapigakura kabla ya ugawaji wa vitambulisho vipya vya kupigia kura.

Alisema Tume imepata mafanikio makubwa ya kukamilisha zoezi la uandikishaji kutokana na ushirikiano walioupata kutoka kwa vyombo vya ulinzi na usalama, viongozi wa vyama vya siasa na serikali pamoja na wananchi wote wa Zanzibar kuwa tayari na kushiriki katika zoezi hilo.

Kwa upande wao, wananchi waliofika katika vituo vya uandikishaji waliipongeza ZEC kwa kuweka utaratibu mzuri wa uandikishaji katika vituo vya uandikishaji na kuwaomba viongozi wa Tume hiyo, kuendelea kuwawekea mazingira mazuri katika hatua zote za uchaguzi ili uchaguzi huo ufanyike kwa uhuru na uwazi.

Wananchi hao waliomba Tume kuendelea kuwaandalia mazingira mazuri ambayo yatawawezesha kushiriki katika uchaguzi mkuu bila usumbufu wowote na kuwataka wananchi wenzao kutodharau fursa wanazopatiwa na viongozi wao katika majimbo ya uchaguzi.

Kazi ya uandikishaji na uhakiki wa taarifa za wapigakura kwa mara ya pili iliyofanyika kwa kuwapa fursa ya kuandikishwa na kuhakikiwa taarifa zao wananchi waliokosa huduma hizo kwa mara ya kwanza imeanza Mei 30, mwaka huu katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na imekamilika Juni 12 katika Wilaya ya Mjini Unguja.

# CUF yaja na bajeti mbadala

**Na Gwamaka Alipipi**

CHAMA cha Wananchi (CUF) kimesema kikiingia madarakani kitajikita katika kuwekeza kwenye kujenga rasilimali watu, kwa kuhakikisha wajawazito na watoto wote wanapata lishe bora.

Kimesema kitahakikisha kundi hilo linapata elimu bora ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutumia kompyuta kwa watoto wote.

Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Prof. Ibrahim Lipumba, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akichambua bajeti ya serikali iliyowasilishwa bungeni mwishoni mwa wiki na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango.

Pamoja na mambo mengine, Prof. Lipumba, alisema CUF itahakikisha huduma za afya za msingi inakuwa ni haki ya wananchi wote.

Alisema kuleta mapinduzi ya kilimo yatakayoongeza ajira na ukuaji wa viwanda, kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa katika kufanikisha malengo ya kutokomeza umaskini katika nyanja zote ifikapo mwaka 2030 itakuwa mojawapo ya agenda.

"Bajeti za CUF ikiingia madarakani itajikita katika kuwekeza kwenye kujenga raslimali watu kwa kuhakikisha wajawazito na watoto wote wanapata lishe bora, elimu bora ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutumia kompyuta kwa watoto wote," alisema Prof. Lipumba.

Aidha, Prof. Lipumba alisema CUF kimeandaa jopo la wataalamu wanaopitia sera ya furaha na haki sawa kwa watu wote, ambayo pamoja na mambo mengineyo imejikita katika utekelezaji wa malengo endelevu ambayo kimsingi yanaunga mkono itikadi ya utajirisho na sera ya haki sawa na furaha kwa wananchi wote.

kuhusu uhusiano kati ya ugonjwa wa corona na bajeti ya serikali mwaka 2020/21, Prof. Lipumba alisema kwa kuwa Tanzania haikuzuia wananchi wasitoke nje, shughuli za kiuchumi ziliendelea kama kawaida.

Alisema uamuzi wa kuwaruhusu wananchi kuendelea na shughuli ulikuwa sahihi ukizingatia kwamba wananchi wengi wanategemea kipato cha kila siku katika sekta siyo rasmi, ili wamudu maisha yao.



Wafanyabiashara katika Soko la Buguruni jijini Dar es Salaam wakisubiri wateja wa kununua machungwa jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanahabari watakiwa tahadhari

**Na Said Hamdani, LINDI**

LICHA ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona kupungua nchini, waandishi wa habari wametakiwa kuchukua tahadhari, ikiwamo kujilinda na maambukizo wanapokuwa katika kutekeleza majukumu yao.

Msisitizo huo umetolewa na Rais wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini (UTPC), Deogratius Nsokolo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa vyombo mbalimbali mkoani Lindi.

Alisema licha ya ugonjwa wa Covid-19 kuonyesha dalili za kupungua nchini, bado upo hivyo ni vizuri kwa wanataaluma hao wakaendelea kuchukua tahadhari ikiwamo kufuata maelekezo kutoka kwa wataalamu wa afya.

Masharti mengine ni kuvaa barakoa, kutumia 'sanitizer' na kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu mmoja na mwingine.

Nsokolo alisema kutokana na umuhimu walionao waandishi kupita maeneo mbalimbali kutafuta taarifa kwa ajili ya kuwapatia wananchi, upo umuhimu mkubwa kuchukua tahadhari ya kujilinda wao wenyewe ili jamii iweze kupata huduma zao za kupata taarifa mbalimbali.

Alisema waandishi wanao wajibu katika kuwatumikia wananchi licha ya uwapo wa changamoto mbalimbali zinazowakabili wakati wa utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

"Hivi sasa UTPC tupo mbioni kuwaleteeni mafunzo yanayohusu ugonjwa huu wa Covid-19 muweze kuripoti vizuri ili jamii ipate uwelewa," alisema Nsokolo.

Rais huyo wa UTPC, amewashauri waandishi ambao hawajafanya maamuzi ya kujiunga na klabu za waandishi ni vema wakafanya hivyo ili waweze kunufaika na matunda yanayotokana na UTPC.

Mwenyekiti wa Klabu ya Mkoa wa Lindi, Christopher Lilai, alisema klabu yao ina wanachama 37, huku saba wakiwa ni wanawake na kwamba wapo baadhi bado hawajajiunga licha ya kuwapa faida zake.

Nsokolo alikuwa na ziara ya kusikiliza changamoto zilizopo na kuongea na waandishi wa vyombo mbalimbali vya habari mkoani hapa.

## Viongozi dini watakiwa kutoa elimu kwa jamii

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

IMEELEZWA kuwa katika mapambano dhidi ya mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia hususan kwa watoto wa kike, viongozi wa dini wana wajibu wa kutoa elimu kwa jamii ili iondokane na matendo hayo ambayo ni chukizo mbele za Mungu.

Hayo yameelezwa na Askofu wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT) Dayosisi ya Mwanza, Philipo Mafuja, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema maandiko matakatifu ikiwamo Bibilia inahitaji viongozi wa dini kuwa sehemu ya kusaidia jamii katika malezi bora ya watoto.

Hivyo alisema wana mchango na wajibu wa kusaidia serikali na jamii kwa katika mapambano ya mimba za utotoni na ukatili kwa kuhakikisha watoto wote hususani wa kike wanalindwa.

## Diwani alia na ubovu barabara

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

KATA ya Mailimoja ni kati ya kata 14 za Halmashauri ya Mji wa Kibaha, ambayo inakabiliwa na changamoto ya ubovu wa barabara za mitaa, hali inayohitaji ukarabati wa mara kwa mara.

Hayo yamebainishwa mwishoni mwa wiki na Diwani wa Mailimoja, Ramadhani Lutambi, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi 2015-2020.

Lutambi alisema ukosefu wa mifereji ya barabara hizo ni kati ya vyanzo vinavyochangia kuharibika mara kwa mara na kupitika kwa shida hasa kipindi cha mvua.

Aidha, hali ya ubovu wa barabara si kwa kata hiyo pekee bali katika maendeleo mbalimbali ya halmashauri hiyo na hivyo kuomba fedha za kutosha kufanya matengenezo makubwa.

Katika hatua nyingine Lutambi alitoa wito kwa vikundi vya wanawake na vijana vilivyonufaika na mikopo ya halmashauri kuhakikisha wanalipa madeni hayo ili vikundi vingine vinufaike.

Alisema baadhi ya vikundi ambavyo vilipatiwa mkopo mwaka 2018 na 2018 hadi sasa havijarejesha na hivyo kukwamisha mipango ya halmashauri kuendelea kutoa mikopo.

## Ujerumani: Wananchi 1,000 wa Syria warejea nyumbani

**BERLIN, Ujerumani**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Ujerumani imesema kuwa tangu mwaka 2017, zaidi ya watu 1,000 wamerejea kwa hiari nchini Syria kupitia ufadhili wa kifedha wa serikali ya Shirikisho.

Ilisema, kuwa ofisi ya Shirikisho ya Uhamiaji na Wakimbizi (BAMF) ililipia safari 199 za kurejea Syria mnamo mwaka 2017, mwaka 2018 safari 466 na mwaka 2019 safari 347. Idadi kamili ya safari hizo za hiari huenda ikawa juu kwa sababu maombi kutoka kwa majimbo yote ya serikali ya Shirikisho la Ujerumani ya kufadhiliwa kwa safari hizo hayajawasilishwa.

Wizara hiyo ilisema kuwa, karibu raia 630,000 wa Syria wametuma maombi ya hifadhi nchini Ujerumani tangu kuanza kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini humo mwaka 2011, huku wengi wakifanikiwa kupata hadhi hiyo ya kuwalinda.

**DW**

## Watafiti wasema China ilipata corona mapema

**WUHAN, China**

UTAFITI umeonyesha kuwa kufurika kwa wagonjwa katika hospitali nchini China kunaashiria kuwa ugonjwa wa corona uliikumba nchi hiyo mapema kabla ya kuripotiwa rasmi.

Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Havard nchini Marekani walisema picha za satelaiti zinaonyesha kuongezeka kwa wagonjwa wengi katika hospitali tano kwenye mji wa Wuhan kuanzia mwisho wa Agosti hadi Desemba.

Walisema ongezeko la wagonjwa wakati huo kunaendana na kuongezeka kwa utafutaji wa taarifa za dalili za kukohoa na kuharisha kipindi hicho hicho.

China imesema kuwa utafiti huo ni dhihaka na uliotegemea taarifa zisizo za kweli. Inaaminika kwamba virusi hivyo vilijitokeza sana China Novemba. Mamlaka nchini China iliripoti visa vya ugonjwa wa mapafu yaani nimonia kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) Desemba 31, mwaka jana.

Watafiti hao walipitia data ya satelaiti katika hospitali tano za Wuhan, kwa kulinganisha na data ya mwisho ya msimu uliopita 2018 hadi kipindi cha mwaka 2019.

Watafiti walibaini magari 171 yakiwa yameegeshwa katika moja ya hospitali kubwa huko Wuhan, Hospitali ya Tianyou Oktoba 2018.

Data ya satelaiti kipindi sawa na hicho 2019 zilizonyesha magari 285 yakiwa katika sehemu hiyo hiyo ikiwa ni ongezeko la asilimia 67.

Walieleza kuwa pia kulikuwa na ongezeka la maneno yaliyokuwa yanatafutwa mitandaoni yanayohusishwa na dalili za virusi vya corona katika mtandao wa Baidu wakati huo.

"Utafiti zaidi bado unahitajika kufanywa kubaini hasa kile kilichotokea na watu kujifunza namna ugonjwa huu ulivyolipuka na hadi ukafika kwa binadamu. Kwa hiyo huu ni ushahidi mwingine," walieleza watafiti hao.

**BBC**

# Mkuu wa Jeshi Polisi ajiuzulu Mmarekani mweusi akiuawa

**WASHINGTON, Marekani**

MKUU wa Jeshi la Polisi wa Jiji la Atlanta nchini Marekani, Erika Shields, alijiuzulu saa chache baada ya Mmarekani mwingine mweusi kuuawa kwa kupigwa risasi na polisi Jumamosi.

Mauaji hayo yametokea wakati polisi walipokuwa wakijaribu kumfanyia kipimo cha kubaini iwapo alikuwa ametumia mihadarati.

Polisi mjini Atlanta walisema kwenye purukushani hiyo mwanaume huyo, Rayshad Brooks, aliinyakua bastola ya kutia ganzi kutoka kwa polisi ambaye alimpiga risasi wakati alipokuwa anakimbia.

Mauaji ya Brooks aliyekuwa na umri wa miaka 27 yamechochea wimbi jipya la maandamano mjini Atlanta, baada ya lile la maandamano ya kupinga kifo cha George Floyd aliyeuawa mjini Minneapolis ambayo kwa sasa yamepungua kasi nchini Marekani na duniani kote.

Meya wa Atlanta, Keisha Lance Bottoms, alitangaza kujiuzulu kwenye mkutano na waandishi wa habari wakati watu wapatao 150 walipoandamana nje ya mgahawa wa Wendy ambako kijana huyo aliuawa Ijumaa jioni.

Meya huyo alitoa wito wa kufutwa kazi mara moja ofisa wa polisi aliyemfyatulia risasi Rayshad Brooks.

Meya huyo ameeleza kuwa hatua ya kujiuzulu kwa mkuu wa polisi wa jiji la Atlanta ni uamuzi wake binafsi na kwamba mkuu mwandamizi wa idara ya kurekebisha tabia, Rodney Bryant, atakaimu nafasi hiyo kwa muda hadi pale mkuu mpya wa polisi atakapopatikana.

***DW***




Baadhi ya raia wa Marekani wakiwa wamebeba mabango wakishinikiza Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kujadili kwa dharura ubaguzi wa rangi na ukatili wa Jeshi la Polisi. **PICHA: ALLIANCE**

# Aweka rekodi kufika kina cha chini baharini

**NEWYORK, Marekani**

MWANAMKE ambaye ni mwanaanga, Dk. Kathy Sullivan (68), amekuwa mtu wa kwanza kufika eneo la kina cha chini baharini.

Dk. Sullivan aliweka historia hiyo kwa kupiga mbizi kwenye mfereji wa Bahari ya Pasifiki ya Mariana wenye urefu wa futi 35,810.

"Nilijihisi kama mgeni anayewasili kwenye sayari nyingine na kusafiri kwenye mwezi kama ilivyo kwa mandhari ya kawaida ya kuvutia. Lilikuwa tukio la kipekee," alisema Dk. Sullivan.

Tukio hilo limemfanya Dk. Sullivan kuwa mtu wa nane na mwanamke wa kwanza kufika katika kina hicho takriban kilomita 11 chini ya sakafu ya Bahari ya Pasifiki.

Dk. Sullivan alitumia muda wa saa 1:30 kutembea katika mfereji huo chini ya bahari ambao ulijengwa kuhimili shinikizo la juu la maji.

Mwekezaji na mvumbuzi, Victor Vescovo, ambaye awali alikuwa wa kwanza kufika kina cha chini cha bahari zipatazo tano alikuwa ameandamana na Dk. Sullivan.

"Sikuwahi kufikiria kwamba iko siku nitapata fursa hii, au Victor atawahi kunitafuta na kunialika kujumuika nae kwenye safari hii," alisema Dk. Sullivan.

Alisema: "Chini ya mifereji kama wa Mariana, maji ni baridi sana, hakuna mwanga, shinikizo la maji chini ni la juu lakini kwa namna moja au nyingine, maisha yanaendelea hata ukiwa huko na sasa hivi watafiti ndiyo wameanza kuchunguza kinachoendelea katika eneo hilo."

Safari ya kwanza kwenda kina cha chini zaidi baharini katika mfereji wa Mariana ilitokea mwaka 1960 na mwanajeshi wa majini wa Marekani, Luteni Don Walsh na mhandisi wa Uswizi, Jacques Piccard.

Nusu karne baadaye, mwelekezi wa filamu, James Cameron, naye akafunga safari ya kwenda eneo hilo mwaka 2012.

Dk. Sullivan alikuwa mwanaanga mwaka 1979 na kuweka historia mwaka 1984 kama mwanamke wa kwanza wa Marekani kwenda anga la mbali na kurejea.

Alitumia muda zaidi ya saa 532 katika anga la mbali, na mwaka 2004 akawa mashuhuri miongoni mwa wanaanga.

Kwa sasa hivi amekuwa mtu wa kwanza kafika katika anga la mbali na kwenda kwenye kina cha chini kabisa cha Bahari ya Pasifiki.

Rob McCallum, mwanzilishi wa shirika lililosaidia katika kutimiza safari ya Dk. Sullivan alisema ni mwanamke mwenye shauku na kujitolea.

***BBC***




# MESSI AENDELEZA REKODI LA LIGA

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi aliweka rekodi nyingine kwenye Ligi Kuu Hispania, La-Liga, Jumamosi wakati Barcelona ilipoibuka na ushindi wakati ligi hiyo ikiwa imerejea tena.

Vinara hao waliibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Real Mallorca kwenye mchezo wa kwanza tangu kusimamishwa kwa ligi hiyo kutokana na mlipuko wa virusi vya corona hapo Machi, mwaka huu.

Arturo Vidal alianza kufunga bao la ufunguzi baada ya dakika mbili tu za mchezo huo, kabla ya Messi kumtengenezea, Martin Braithwaite aliyefunga bao la pili na la kwanza kwake tangu atue Barca.

Halafu Jordi Alba akafunga bao la tatu baada ya kufanya kazi ya ziada na kuendelea kuipa uhakika Barcelona.

Yeye Messi alifunga la nne katika muda wa majeruhi na hivyo kufikisha mabao 20 LaLiga aliyofunga hadi sasa kwenye msimu huu wa 2019-20.

Nyota huyo wa Argentina ni mchezaji pekee kufunga mabao 20 au zaidi kwa kila msimu katika misimu 12 mfululizo.



## GATTUSO ASHUKURU WACHEZAJI NAPOLI

**NAPLES, Italia**

GENNARO Gattuso aliwashukuru wachezaji wa Napoli kwa kucheza kwa "kiwango cha kuvutia" baada ya kupata sare na Inter Milan na kutinga fainali ya Kombe la Coppa Italia.

Dries Mertens aliweka rekodi ya kuwa mfungaji wa wakati wote wa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Italia, Serie A, baada ya kusawazisha bao la Christian Eriksen kwenye mchezo huo wa Jumamosi uliomalizika kwa sare ya kufungana bao 1-1 kwenye dimba la San Paolo.

Matokeo hayo yalitosha kuipeleka Napoli kwenye fainali ambapo itacheza na Juventus iliyoshinda kwa uwiano wa mabao 2-1 kwenye nusu fainali.

Gattuso alitoa ushindi huo kwa dada yake, Francesca aliyefariki mapema mwezi huu akiwa na umri wa miaka 37.

"Nayatoa matokeo haya kwa dada yangu na familia yangu," alisema kupitia tovuti ya klabu hiyo.

"Vijana walicheza kwa kiwango cha kuvutia sana na walijitolea wakiwa uwanjani. Nawashukuru wao kwa sababu walicheza kwa sababu yangu na pia kwa ajili ya timu.

"Nina timu ambayo ina wachezaji wenye ubora, lakini walicheza kwa kujituma na kuhakikisha wanaibuka na ushindi."

Napoli sasa itacheza na Juventus kwenye fainali itakayopigwa mjini Rome Jumatano.

# BAYERN BADO POINTI TATU KUBEBA TAJI BUNDESLIGA

**MUNICH, Ujerumani**

HANSI Flick amewaambia nyota wake wa Bayern Munich kwenda kumaliza kazi kwa Bremen hapo kesho baada ya kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kulibeba taji la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu.

Kocha huyo mkuu, ambaye alichukua mikoba kutoka kwa Niko Kovac Novemba mwaka jana, alipata ushindi wa 25 katika mechi 28 kama kocha wa Bayern, shukrani kwa Leon Goretzka aliyeipa ushindi Jumamosi.

Ilipata ushindi wa 2-1 dhidi ya Borussia Monchengladbach kwenye mchezo huo na sasa Bayern inahitaji ponti tatu tu kutangazwa mabingwa.

Hiyo inamaana kwamba, sasa Bayern wanaongoza msimamo kwa pointi saba dhidi ya Borussia Dortmund waliopo nafasi ya pili, na zikiwa zimesalia mechi tatu ligi kumalizika.

Ushindi dhidi ya Werder Bremen pale kwenye Uwanja wa Weserstadion kesho Jumanne utawafanya watwae ubingwa wa Bundesliga kwa mara ya nane mfululizo.

"Tunatakiwa kuendelea kuweka umbali kwa ushindi, hilo linanifanya mimi niwe na furaha sana," amesema Flick.

"Kule Bremen tunataka kupata ushindi na kuendelea kupata mafanikio, hivyo ni wakati mzuri na tunatakiwa kwenda kumaliza kazi."





# POGBA

## ATABAKI UNITED, ASEMA JANUZAJ

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba hataondoka Manchester United msimu unaokuja wa dirisha la uhamisho, licha ya uvumi kuzidi kuendelea kuhusu majaliwa yake, kwa mujibu wa kiungo na rafiki yake wa karibu, Adnan Januzaj.

Pogba, ambaye alicheza pamoja na Januzaj kwenye akademi ya kukuza vipaji vya wachezaji vijana ya United, alirudi kwenye klabu hiyo ya Ligi Kuu England akitokea Juventus mwaka 2016, kwa ada iliyoweka rekodi ya duniani ya pauni milioni 90.

Hata hivyo, shutuma zimekuwa zikumwandama kutokana na kushindwa kuonyesha thamani ya fedha hiyo, huku kiwango chake kikiwa cha kushuka na kupanda.

Matatizo ya majeruhi ya mara kwa mara yamemfanya nyota huyo wa Ufaransa kucheza mechi saba tu za Ligi Kuu msimu huu, huku yeye na wakala wake, Mino Raiola hajaonyesha aibu kudokeza kuhusu mpango wa kuondoka.

Lakini United imeripotiwa kwamba itapambana kuhakikisha inambakiza Pogba, huku mchezaji mwenzake wa zamani, Januzaj, ambaye kwa sasa anacheza kule Real Sociedad, anajiamini kwamba kiungo huyo atabakia pale Old Trafford.

Akizungumza na Het Nieuwsblad, Januzaj amesema: "Nafikiri atabakia. Paul na mimi bado tupo karibu sana.

"Tumejuana kwa muda mrefu tangu tukiwa watoto tulikuwa pale kwenye akademi ya United. Familia zetu pia ni marafiki na tunawasiliana mara kwa mara. Hili halitaweza kubadilika."

Pogba amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Real Madrid ambapo mkataba wake wa sasa unamalizika mwakani, ingawa ana kipengele cha kuongeza hadi mwaka 2022.

## PSG YAWARUHUSU SILVA, CAVANI KUONDOKA

**PARIS, Ufaransa**

PARIS Saint-Germain imeamua kuwaachia nahodha, Thiago Silva na mfungaji wa rekodi ya wakati wote klabu hapo, Edinson Cavani, Mkurugenzi wa Michezo, Leonardo amebainisha.

Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, ilifutwa kwa msimu huu Aprili, lakini PSG wana matumaini wachezaji hao wawili watabakia kwa ajili ya mechi zilizobaki kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa mujibu wa jarida la Le Journal du Dimanche, Leonardo anaamini muda sasa umefika kwa PSG kuachana na wachezaji hao ambao walikuwa nguzo ya mafanikio kwa klabu hiyo.

Silva alijiunga nao akitokea Milan mwaka 2012 na amekuwa nguzo ya mafanikio kwenye safu ya ulinzi ya PSG, huku mshambuliaji Cavani alisajiliwa akitokea Napoli mwaka 2013 na amefunga mabao 200 kwa klabu hiyo.

Gazeti hilo lilimnukuu Leonardo akisema kwamba, kukaa kwao hapo "kunakaribia mwisho", huku wachezaji wote wataondoka wakiwa huru baada ya mikataba yao kumalizika.

"Yalikuwa maamuzi magumu kuyafanya," amesema Leonardo.

"Wachezaji wote wametoa mchango mkubwa katika historia ya klabu: Tulikuwa na shauku ya kutaka kuendelea nao, lakini sasa haina namna wataondoka."

Mlinzi wa kimataifa wa Brazil, Silva atatimiza umri wa miaka 36 Septemba, mwaka huu, huku mshambuliaji wa kimataifa wa Uruguay, Cavani atatimiza miaka 34 Februari mwakani.

## MOURINHO: SPURS HAITACHEZA MECHI ZA KIRAFIKI

**LONDON, England**

JOSE Mourinho anaamini ni "hatari kubwa" kwa Tottenham Hotspur kucheza mechi zaidi za kirafiki kabla ya kurudi kwa Ligi Kuu England.

Spurs ilifurahia mazoezi kwa mechi ya kirafiki dhidi ya Norwich City Ijumaa, mchezo ambao ulikuwa ukicheza kwa mapumziko mare nne kwa dakika 30, wakati wachezaji wa klabu zote mbili wakijaribu kujifua kurudisha viwango vyao.

Harry Kane, Moussa Sissoko, Son Heung-min na Steven Bergwijn -ambao walikuwa majeruhi kabla ya mlipuko wa virusi vya corona, wote walikuwapo.

Mourinho angependa kupata mchezo mwingine kabla ya Ijumaa dhidi ya timu yake ya zamani ya Manchester United, lakini bado hajajiandaa kucheza kamari kwa wachezaji wake.

"Hatuwezi kuwa tena na mchezo wowote wa kirafiki. Tunafikiri itakuwa vizuri, lakini ni hatari sana kucheza tena kwa wachezaji wangu," alisema Mourinho akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Tutafanya mazoezi ya kawaida wiki hii, kuanzia Jumatatu (leo) hadi Ijumaa. Baada ya hapo tutakuwa na siku mbili zaidi na halafu kucheza na West Ham, hivyo siku 10 zijazo tutakuwa bize."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL YAKARIBIA KUMNASA UPAMECANO

●●●Ni beki ambaye anawindwa na klabu mbalimbali za Ulaya ikiwamo United, Bayern, Milan...

**MILAN, Italia**

KLABU ya RB Leipzig imewajulisha AC Milan kuwa Arsenal inakaribia kuibuka kidedea katika mbio za kuwania saini ya beki wake, Dayot Upamecano, taarifa zilizopatikana Italia zimeandika.

Kiwango cha beki huyo wa kati Mfaransa kimezivutia klabu mbalimbali kubwa za Ulawa ikiwamo Manchester United na Bayern Munich baada ya kuwa na msimu mzuri kwenye Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga.

Vigogo wa Serie A, Milan walipanga kumsajili Upamecano kwa lengo la kupata mrithi wa muda mrefu wa nahodha wao, Alessio Romagnoli, huku hatima ya nyota wa Sevilla, Simon Kjaer ambaye yuko kwa mkopo klabuni hapo na ambaye mkataba wake wa kuitumikia klabu hiyo ya San Siro mwishoni mwa msimu huu haijulikani.

Lakini kwa mujibu wa gazeti la Tuttosport, Milan imejulishwa na klabu hiyo ya Bundesliga, Leipzig kuwa beki huyo mwenye umri wa miaka 21 anajiandaa kujiunga na kikosi cha Mikel Arteta.

Taarifa ziliendelea kudai kwamba kocha huyo alifanikiwa kuingia makubaliano na klabu hiyo ya Ujerumani ingawa beki huyo tayari alikuwa kwenye list ya nyota watakaosajiliwa na Ralf Rangnick.

Habari zaidi huko Italia zinasema kuwa Mkuu wa Kitengo cha Soka wa sasa wa Leipzig anajiandaa kuchukua nafasi ya Kocha Stefano Pioli mwishoni mwa msimu huu na atamjumuisha Upecano kuwa mmoja wa nyota wa kikosi cha Julian Nagelsmann.

Ripoti hiyo tajwa imeanza kusambaa baada ya Nagelsmann kukiri beki huyo mwenye umri wa miaka 21 alianza 'kuvurugwa' kufuatia uvumi ataondoka Red Bull Arena.

Beki huyo alitolewa nje wakati timu yake ikitoka sare ya bao 1-1 wikendi iliyopita walipokuwa nyumbani waliivaa Paderborn na alisimamishwa wakati klabu yake ikishinda magoli 2-0 dhidi ya Hoffenheim.

"Ni beki mwenye uwezo. Anajua kuzuia kwa kiwango cha juu, hata kama atakuwa amechelewa," alisema Nagelsmann kabla ya mchezo huo wa Ijumaa.

"Binafsi anajuwa kama siku hizi hachezi katika kiwango cha juu. Yeye ni mchezaji kijana ambaye anahusishwa na kutakiwa na klabu za juu.

"Ni jambo la kawaida kwake kuwa na uwezo mdogo wa kukabiliana na changamoto," aliongeza.

## KWA UFUPI

**SANCHO KUBAKI DORTMUND**

KOCHA wa Borussia Dortmund, Sebastian Kehl, amekanusha uvumi kuhusiana na tetesi za nyota wake, Jadon Sancho (20), kujiunga na Liverpool ifikapo majira ya joto. Manchester United pia inatajwa kumwania mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya England. ***(Sunday Mirror)***

**WERNER NJIA NYEUPE**

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, amesema Timo Werner hayuko tena kwenye mipango ya kubakia na klabu hiyo na sasa mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ujerumani mwenye umri wa miaka 24, anasubiri kukamilisha mchakato wa kujiunga na Chelsea. ***(Sunday Mirror)***

**ARRIZABALAGA MAJARIBUNI**

NYOTA Kepa Arrizabalaga amebakiza mechi tisa za kuamua hatima yake ndani ya kikosi cha Chelsea, idadi kubwa ya wachezaji inatajwa kuja kumrithi golikipa huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Sunday Express)***

**JORGINHO ATAJWA JUVE**

JORGINHO na Kocha wa Juventus, Maurizio Sarri hawajawahi kuzungumza tangu mwalimu huyo alipoondoka Chelsea, lakini kiungo huyo mwenye umri wa miaka 28 anahusishwa na mpango wa kutua kwa vigogo hao wa Serie A. ***(Mail on Sunday)***

**EDOUARD AIKACHA ARSENAL**

STRAIKA wa Celtic, Odsonne Edouard amekanusha uvumi wa kuhamia Arsenal, nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, amesema anataka kuwa sehemu ya kikosi kitakachotwaa ubingwa wa ligi kwa mara ya 10 mfululizo akiwa na klabu hiyo ya Scotland. ***(Mail on Sunday)***

**JUVE, DYBALA KITAELEWEKA**

MABOSI wa Juventus wanaamini watafanikiwa kumsainisha mkataba mpya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Paulo Dybala (26), ambaye anataka kulipwa kiasi cha pauni milioni 11 kwa mwaka kwenye dili hilo jipya. ***(Goal)***

**MAINZ YAMTAKA AWONIYI**

KOCHA wa Mainz, Rouven Schroder, amesema klabu iko katika mazungumzo ya kumbakisha klabuni hapo mshambuliaji wa Liverpool, Taiwo Awoniyi. Mnigeria huyo mwenye umri wa miaka 22 yuko kwa mkopo katika timu hiyo inayoshiriki Bundesliga tangu majira ya joto mwaka jana. ***(Goal)***

**VIDAL KUONDOKA BARCA**

KIUNGO wa Timu ya Taifa ya Chile, Arturo Vidal (33), ameshauri ni vyema akajiunga na Inter Milan, na kusema haoni kama ana nafasi kwenye kikosi cha Barcelona. ***(Goal)***

**CAVANI, SILVA SAFARI IMEIVA**

STRAIKA Edinson Cavani (33), ataondoka Paris St-Germain sambamba na beki, Thiago Silva (35), ifikapo Agosti mwishoni, Mkurugenzi wa Michezo wa klabu hiyo amethibitisha. ***(Le Journal du Dimanche)***

**MOURINHO AMKATAA NDOMBELE**

WAKATI Tanguy Ndombele akiwa amebakisha muda wa mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Tottenham, ameshindwa kumshawishi kocha wa klabu hiyo, Jose Mourinho. Mfaransa huyo alinunuliwa kwa dau la pauni milioni 52 akitokea Lyon. ***(Soccernet)***

**SANCHEZ SOKONI ULAYA**

MSHAMBULIAJI Alexis Sanchez ambaye bado ni mali ya Manchester United huenda akasaini mkataba wa kudumu na Inter Milan, lakini anatajwa akawa sehemu ya mchakato wa kufanikisha mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho au beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly wanatua United.

HABARI MICHEZO

# EYMAEL AMVULIA KOFIA YONDANI, KASI IMERUDI

**Na Isaac Kijoti, SHINYANGA**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, ameeleza kufurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na beki kisiki wa timu hiyo, Kelvin Yondani, katika mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Mwadui FC.

Yondani, ambaye tangu kutua kwa Eymael amekuwa si chaguo lake katika kikosi cha kwanza, juzi alianzishwa akicheza kama kiungo mkabaji, namba sita dhidi ya Mwadui FC na kuonyesha uwezo mkubwa uliowasaidia kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Akimzungumzia beki huyo, ambaye amekuwa akiwashuhudia Juma Makapu na Lamine Moro wakimsughulisha benchi, Eymael alisema Yondani ameonyesha ubora wa hali ya juu kwa kucheza vizuri katika nafasi tofauti.

"Kelvin kacheza vizuri katika nafasi ya kiungo, kinachotakiwa kwake kwa sasa ni kubadilika na kuelekeza akili yake mchezoni, kaonyesha anaweza kuwa msaada kwa kucheza nafasi zaidi ya moja uwanjani," alisema Eymael. Katika mechi hiyo ya kiporo cha Ligi Kuu iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Kumkumbu ya Kambarage mjini Shinyanga, bao hilo pekee la Yanga liliwekwa kimiani na Mapinduzi Balama dakika ya sita akiitendea haki pasi aliyorudishiwa na Deus Kaseke.

Yondani akisaidiana na mabeki wa kati, Lamine Moro na Juma Makapu, waliweza kuidhibiti vema safu ya ushambuliaji ya Mwadui FC ambayo ilionyesha uhai mkubwa dakika 15 za mwanzo za kipindi cha pili.

Yanga itashuka tena dimbani keshokutwa, Jumatano safari hii ikiwa ni katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kuwakabili JKT Tanzania na licha ya Eymael kuahidi kunaweza kuwa na mabadiliko kidogo katika kikosi chake, kwa sifa alizozitoa kwa Yondani ni wazi anaweza kumwanzisha tena.



Mchezaji wa Kitunda FC, Kelvin Peter (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa Relini FC, Rashid Haji, katika mchezo wa kirafiki uliochezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda jijini, Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Mwadui aigeukia Simba

**Na Isaac Kijoti, SHINYANGA**

HUKU akieleza likizo ya muda mrefu ya virusi vya corona ni moja ya sababu ya kupoteza mechi yao ya kwanza tangu kurejea kwa Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Mwadui FC, Khalid Adam, amesema akili yao kwa sasa ni mchezo ujao dhidi ya Simba.

Ikiwa katika uwanja wao wa nyumbani wa CCM Kambarage, Mwadui FC juzi ilipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Yanga, huo ukiwa ni mchezo wa kwanza kuchezwa tangu ligi hiyo iliposimama Machi 17, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Adam alisema kukaa muda mrefu bila kucheza mechi yoyote ni moja ya sababu kwa wachezaji wake kushindwa kwenda na kasi ya mchezo.

Hata hivyo, kocha huyo alisema wachezaji wake walijitahidi ila walipoteza nafasi nyingi na wapinzani wao wakawa makini kuitumia nafasi moja waliyoipata.

"Kikubwa naamini mchezo ujao (dhidi ya Simba) wachezaji watakuwa wamezidi kuimarika na kufanya vizuri," alisema kocha huyo ambaye akiwa na kikosi chake hicho wanashikilia rekodi ya kuwa timu ya kwanza kuifunga Simba msimu huu.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza Simba ikiwa katika Uwanja wa CCM Kambarage ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mwadui.

Simba ambayo inaongoza msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 71, kabla ya mchezo wao wa jana dhidi ya Ruvu Shooting, itashuka kwenye Uwanja wa Taifa Jumamosi kuwakaribisha wababe wao, Mwadui FC.

## JKT Tanzania yaitisha Yanga

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Mohammed Abdallah 'Bares' amesema kikosi chake kipo imara na kuwatahadharisha Yanga wasitarajie mteremko katika mchezo wao utakaochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma.

Akizungumza na Nipashe jana, Bares alisema hakuna mechi rahisi na kwa upande wake wanajipanga kupambana kutafuta pointi tatu kwa ajili ya kuvuna pointi na kujiweka katika nafasi nzuri zaidi kwenye msimamo.

Bares alisema wanaiheshimu Yanga kwa sababu ni timu kongwe na yenye wachezaji na makocha wazoefu, lakini wao wamejipanga kutafuta ushindi kwenye uwanja wa nyumba.

"Yanga tunawaheshimu, tumejipanga kupambana kutafuta ushindi katika kila mechi, kwa sababu nafasi ya sasa na pointi 41 tulizokuwa nazo, zinaweza kufikiwa na timu zilizopo chini yetu, hivyo kila mmoja jukumu lake kutafuta ushindi," alisema Bares.

Aliongeza ushindi ndio jambo pekee wanalolifikiria katika mchezo huo wa keshokutwa na mingine itakayofuata kwenye ligi hiyo.

"Ukizingatia msimu huu timu nyingi zitashuka daraja, kila aliyekuwa chini yetu anahitaji nafasi yetu, kila mtu anahitaji kushinda mechi zake kuongeza pointi ambazo zitamweka mahali salama na kumwepusha na janga la kushuka daraja," aliongeza kocha huyo.

## Namungo walia na 'upepo mbaya'

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, amesema 'upepo' haukuwa upande wao hivyo hawezi kuitupia lawama safu yake ya ulinzi baada ya washambuliaji wa Coastal Union kusawazisha mabao yote mawili katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliochezwa juzi.

Namungo ilishindwa kulinda ushindi wao wa mabao 2-0 hadi walipokwenda mapumziko wakiongoza dhidi ya Coastal Union na kuruhusu wenyeji wakasawazisha magoli hayo, matokeo ya mwisho ikiwa ni sare ya 2-2.

Hitimana aliliambia gazeti hili timu yote inastahili lawama kwa kushindwa kuzuia ushindi huo walioupata na kamwe hawezi 'kuwabebesha mizigo' mabeki wake pekee.

Kocha huyo alisema mabeki wao wako sawa na suala la kwenda hadi mapumziko wakiwa mbele na wenyeji kufanikiwa kusawazisha ni jambo la bahati. "Kufungwa magoli ni timu nzima na si walinzi, tuna muda mrefu hatujacheza pia kukosa wachezaji wengi wa kati pamoja, na kugundua mapungufu yetu imechangia wenyeji wetu kutumia vema kusawazisha idadi hiyo ya mabao," alisema Hitimana.

Aliongeza wanayaweka pembeni mawazo ya matokeo ya mchezo huo uliopita na sasa wanajiimarisha na maandalizi ya mechi ijayo dhidi ya Kagera Sugar itakayochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Kassim Majaliwa.

Michezo
Jumatatu Juni 15, 2020
Nipashe



Arsenal yakaribia kumnasa Upamecano

HABARI UK 22



Mshambuliaji wa Simba, John Bocco (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Ruvu Shooting, Zuberi Badi, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# SIMBA SC, RUVU HAKUNA MBABE

## ●●●Ni katika mbio za kuwania ufalme wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kichuya aanza kufanya...

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa na Fully Maganga wa Ruvu Shooting dakika ya 31, jana liliinyima Simba ushindi kwenye mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya mapumziko ya kupisha janga la ugonjwa wa Covid-19, unaoletwa na virusi vya corona.

Maganga aliunganisha mpira wa kona kwa kichwa uliopigwa na Abdulrahman Mussa, huku mabeki wa Simba wakijichanganya wenyewe na kumpa nafasi mfungaji kuisawazishia timu yake.

Kabla ya bao hilo, Simba ilikuwa ikiongoza kwa bao 1-0 lililowekwa wavuni na mchezaji mkongwe na timu hiyo, Shiza Kichuya dakika ya 11 akimalizia mpira uliotemwa na kipa Mohamed Makaka, baada ya kushindwa kudaka shuti alilopiga yeye mwenyewe akiunganisha krosi ya Meddie Kagere.

Katika mechi hiyo, Simba haikuonekana tishio sana kwa Ruvu Shooting ambayo katika kipindi cha kwanza, Maafande hao walianza mechi hiyo kwa kasi na kuelewana kwa muda mrefu.

Sekunde ya 25 tu Abdurahman Mussa alipiga mpira mrefu ambao ulitoka kidogo ya lango la Simba.

Wakati Simba ikiendelea kuzubaa, Mussa tena aliingia ndani ya eneo la hatari la Simba na kuachia shuti lililodakwa na kipa Aishi Manula dakika ya 10.

Hassan Dilunga aliikosesha Simba bao dakika ya 23 alipopewa pande safi, lakini alijikwaa mwenyewe na kuanguka.

Alikuwa ni Dilunga tena ambaye hakuwa kwenye kiwango kizuri jana, alipokosa bao kwa kupiga shuti kubwa akiwa amebakia na kipa Makaka ndani ya eneo la hatari.

Kipindi cha pili Simba iliwatoa Kichuya, Luis Miquissone, Gadiel Michael na Dilunga, nafasi zao zikachukuliwa na Deo Kanda, Francis Kahata, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na Miraji Athumani, ambao yalichangia kuleta 'uhai' kwenye timu kuanzia dakika ya 70 hadi mwisho wa mchezo, lakini hayakubadilisha matokeo.

Hata hivyo safu ya ulinzi ya Ruvu Shooting, ikiongozwa na Omari Kindamba, Kassim Simbaulanga, Baraka Mtuwi, Zuberi Dabi na golikipa wao Makaka ambaye alifanya kazi ya ziada kuzuia michomo ya kina Kagere na John Bocco, ilifanya vema kwenye mchezo huo.

Kwa matokeo hayo, Simba bado inaendelea kuongoza ligi, ikiwa imeongeza pointi moja na kufikisha 72, ikicheza mechi 29, huku Ruvu Shooting ikifikisha pointi 40 na kwenye msimamo ikikamata nafasi ya 11 baada ya kushuka dimbani michezo 29.

Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena keshokutwa kwa JKT Tanzania kuikaribisha Yanga kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.

Simba; Aishi Manula, Shomari Kapombe, Gadiel Michael, Erasto Nyoni, Paschal Wawa, Mzamiru Yassin, Dilunga, Miquissone, Kagere, Bocco na Kichuya.

Ruvu Shooting; Mohamed Makaka, Omar Kindamba, Kassim Simbaulanga, Baraka Mtuwi, Zuberi Dabi, Abulrahman, Shaaban Msala, Ghaham Maftah, Fully Maganga na William Patrick.

# Eymael: Nafasi ya pili muhimu

**Na Isaac Kijoti, SHINYANGA**

KIWANGO kilichoonyeshwa na wachezaji wake dhidi ya Mwadui FC wakitokea kwenye mapumziko ya corona, kimemkuna Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael na kueleza "nina matumaini makubwa tunaweza kumaliza nafasi ya pili".

Yanga jana ilicheza mechi ya kwanza tangu Ligi Kuu isimame Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Katika mechi hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mjini Shinyanga, Yanga iliibuka na ushindi wa bao 1-0 shukrani zikimwendea Mapinduzi Balama aliyeukwamisha mpira wavuni dakika ya sita baada ya kuonana vema na Deus Kaseke.

Akizungumza na Nipashe baada ya mchezo huo, Eymael alisema kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake kimempa matumaini ya kufanya vizuri katika mechi zilizobaki.

Eymael, ambaye alijiunga na timu hiyo siku moja kabla ya mechi, alisema licha ya mapumziko ya muda mrefu bila kucheza, wachezaji wake walicheza vizuri jambo ambalo limampa matumaini ya kumaliza nafasi ya pili.

"Kuna mambo madogo madogo yakuyafanyia kazi, naamini mechi zijazo wachezaji watazidi kuimarika na kuonyesha kiwango bora zaidi," alisema.

Akizungumzia mechi yao ijayo dhidi ya JKT Tanzania itakayopigwa kesho kutwa Jumatano katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, Eymael alisema kikosi chake kinaweza kuwa na mabadiliko machache ya kiufundi.

Mbelgiji huyo alisema wachezaji wote wapo vizuri isipokuwa, Jaffar Mohamed ambaye alipata majeraha, lakini kwa mujibu wa daktari wa timu hakuumia sana na anaweza kuanza mazoezi mepesi.

Kwa matokeo hayo, Yanga ambayo iliondoka mjini hapa jana asubuhi kuelekea Dodoma tayari kwa mchezo wao dhidi ya JKT Tanzania, inaendelea kushika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 54 ikizidiwa tu kwa tofauti ya mabao na Azam FC ambayo jana usiku ilikuwa ikiikaribisha Mbao FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >